SUPA JACKPOT
TZS.1,096,041,286
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Papa** Francis atoka hospitalini, afya yake yaimarika

UKURASA 17




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 2, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581268
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Askari polisi mbaroni kwa mauaji dereva bodaboda

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3



### OTHMAN ATAKA MFUNGO RAMADHANI KUWA ELIMU KATIKA KUTENDA MEMA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni vyema kwa viongozi wenye dhamana katika nafasi mbalimbali, kuyafanyia kazi kwa ...

UKURASA WA 4

### RAS AWAANGUKIA WALIMU MAPAMBANO USHOGA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, amewataka walimu kusaidia kupambana na tatizo la mapenzi ya jinsia...

UKURASA WA 5

### MOI YAFANYA UPASUAJI WATOTO VICHWA VIKUBWA



TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), imefanya upasuaji kwa watoto wawili wenye vichwa vikubwa, kupitia kambi maalum ya matibabu ya kibingwa na bobezi inayoendeshwa na madaktari bingwa...

## Wasiojulikana wavamia msikiti, wapora vitu na kuua mlinzi

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto) akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Abdallah Shaib Kaim, baada ya kuuwasha jana katika Uwanja wa CCM Nangwanda Sijaona, Mtwara. **PICHA:OWM.**

# Waziri Mkuu awapa kibarua ma-RC wa mikoa 12 udumavu

UK. 2

MICHEZO YANGA, MAZEMBE HESABU UWANJANI UK. 24 MAONI, KATUNI UK.6

# Askari polisi mbaroni kwa mauaji dereva bodaboda

**Na Samson Chacha,** TARIME

JESHI la Polisi, Mkoa wa Kipolisi Tarime/ Rorya linamshikilia askari wake wa Kituo cha Sirari, Samwel Kuleletela, kwa madai kumpiga risasi dereva bodaboda, Ngondi Masiaga (22) sehemu ya paja na kusababisha kifo chake

Kamanda wa Polisi mkoa huo, Kamishna Msaidizi (ACP) Geofrey Sarakikya, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitolea mpakani Kitongoji cha Nyansisina Kijiji cha Kubiterere, Kata ya Mwema Tarafa ya Inchugu.

Akielezea mkasa wa tukio hilo, Kamanda Sarakikya alisema askari huyo na mwenzake walikuwa doria na waliwasimamisha waendesha bodaboda waliokuwa wamebeba mifuko ya saruji ambayo walikuwa wanaingiza nchini kutokea Kenya ikidaiwa haikulipiwa ushuru.

"Katika majibizano yao kati ya bodaboda huyo na askari huyo (Samwel) ilisababisha askari kumpiga risasi mbili dereva huyo wa bodaboda (Ngodi) sehemu ya paja na kusababisha kutokwa damu nyingi na kupoteza maisha kabla hajafikishwa katika hospitali ya wilaya kupatiwa matibabu," alisema.

Alisema kwa sasa wanamshikilia askari huyo kwa mahojiano zaidi kwa kosa la mauaji, huku akisisitiza kuwa Jeshi la Polisi limekuwa likitoa mafunzo na elimu kwa askari kutotumia nguvu zaidi katika ukamataji na kuangalia ukubwa wa kosa.

Kamanda Sarakikya alisema hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa askari huyo, huku akitoa onyo kwa askari wengine wanaovunja sheria.

Baba wa marehemu, Marwa Masiga, akizungumza na waandishi wa habari alisema: "Nimempoteza kijana wangu tuliyekuwa tunamtegemea mimi na familia yangu kutokana na biashara yake ya ujasiriamali. Alikuwa anatusaidia kujikwamua na maisha wakiwamo wadogo zake."

Alisema mifuko mitano ya saruji aliyokuwa amebeba alikuwa amenunua kihalali na kwamba alikuwa anakuja kufanya biashara hapa nchini.

"Saruji ambayo kijana wangu alikuwa ameibeba alikuwa amenunua, faida ya mfuko mmoja ni Sh. 2,000, kwa mifuko mitano aliyobeba alikuwa anapata faida ya Sh. 10,000, yaani faida ya Sh. 10,000 imemuua kijana wangu. Naomba serikali itusaidie na kumchukulia hatua askari huyo," alisema Marwa.

Baadhi ya wakazi wa vijiji vya Kubiterere, Nyamohonda, Borega, Ikoma na Kogaja, wamelaani kitendo cha askari huyo kumpiga risasi bodaboda huyo na kusababishia kifo.

Wakizungumza na Nipashe pasipo kutaja majina yao, wakazi hao walisema Ngondi alikuwa kijana mdogo, hivyo waliiomba serikali kufanya uchunguzi kwa askari wa vituo vya mipakani kwa madai kwamba wengi wao hawafuati maadili ya kazi, wanakiuka sheria na kuleta migongano kwa jamii na jeshi hilo.



Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto Kanda ya Ilala, Michael Bachubira, akizungumza na baadhi ya wakazi wa kanda hiyo, alipokuwa akitoa elimu kuhusu majanga ya moto juzi, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri Mkuu awapa kibarua ma-RC wa mikoa 12 udumavu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka Wakuu wa Mikoa 12 yenye viwango vya juu katika udumavu, kuchukua hatua stahiki kutatua tatizo hilo kutokana na kuzidi wastani wa kitaifa kwenye mikoa yao na kuhimiza lishe bora.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wakazi wa Mtwara na mikoa ya jirani waliofika kushuhudia uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa uliofanyika kwenye uwanja wa CCM Nangwanda Sijaona, Manispaa ya Mtwara.

"Mikoa yenye kiwango kikubwa cha udumavu zaidi ya wastani wa kitaifa ni Iringa inayoongoza kwa asilimia 56.9, Njombe (asilimia 50.4), Rukwa (asilimia 49.8), Geita (asilimia 38.6) Ruvuma (asilimia 35.6), Kagera (asilimia 34.3), Simiyu (asilimia 33.2), Tabora (asilimia 33.1), Katavi (asilimia 32.2), Manyara (asilimia 32), Songwe (asilimia 31.9) na Mbeya (asilimia 31.5). Viongozi wa Mikoa hii waitafakari hali hii na kuchukua hatua stahiki," alisema.

"Taarifa zilizopo zinaonyesha hali ya lishe miongoni mwa Watanzania hairidhishi kutokana na kuathiriwa na tatizo la udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, uzito pungufu, ukondefu na uzito uliozidi pamoja na uliokithiri (kiribatumbo)," aliongeza.

Pia alisema hali ya uzito uliozidi na uzito uliokithiri (kiribatumbo) ndicho kiashiria pekee ambacho hakijawahi kupungua na kimeendelea kuongezeka kutoka asilimia 11.3 mwaka 1991 hadi asilimia 31.7 mwaka 2018 kwa Tanzania Bara na kwa Zanzibar imefikia asilimia 41.8 katika kipindi hicho hicho.

Tatizo la uzito uliozidi na kiribatumbo, alisema ni kubwa katika mikoa ya Kilimanjaro ambako ni asilimia 49, Dar es Salaam (asilimia 48.6), Mjini Magharibi (asilimia 47.4) na Kusini Unguja (asilimia 39.4).

"Hali hii inaelekea kuwa janga la kitaifa na kisababishi kikubwa cha kuongezeka baadhi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kisukari, saratani na magonjwa ya moyo.

"Wananchi wenzangu, sasa ni wakati muafaka wa kubadili mitindo ya maisha yetu kwa kufanya mazoezi angalau nusu saa kila siku na kula mlo kamili sambamba na kuepuka vyakula vyenye mafuta mengi, sukari nyingi, pombe na sigara," alisisitiza.

Mwenge wa Uhuru utakimbizwa kwenye mikoa yote 31 na halmashauri 195 kwa siku 196. Waziri Mkuu aliuwasha mwenge huo saa 6.06 mchana na saa 6.07 akamkabidhi Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Abdallah Shaib Kaim (anayetoka Kaskazini Pemba). Saa 6.08 Shaib alikiri kupokea mwenge huo na kuahidi kuwa ataukabidhi kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ifikapo Oktoba 14, mwaka huu ukiwa salama.

Wakimbiza mwenge wengine na mikoa wanayotoka ni Martin Mkanga (Mtwara), Atupokile Mhalile (Dodoma), Zainab Hemed Mbetu (Kusini Unguja), Emmanuel Hondi (Manyara) na Juma Silima Sheha (Kaskazini Unguja).

Kaulimbiu ya mwaka huu imelenga maeneo makuu sita yakiwemo ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira, mapambano dhidi ya rushwa, UKIMWI, dawa za kulevya, malaria na lishe bora.

Ujumbe maalum wa mbio hizo ni "Umuhimu wa Kuhifadhi Mazingira na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji kwa Ustawi wa Viumbehai na Uchumi wa Taifa."

Mbio za mwenge wa uhuru ziliasisiwa mwaka 1961 na Baba wa Taifa, Hayati Julius K. Nyerere ikiwa ni ishara ya kuwepo kwa Taifa huru la Tanganyika.

Na umekuwa ukikimbizwa katika mikoa yote ili kuhamasisha amani, uzalendo, umoja na mshikamano.

**DHAMIRA YA SERIKALI**

Waziri Mkuu alisema dhamira ni kuboresha huduma za kijamii na maisha ya Watanzania katika sekta za elimu, afya, maji na barabara. Hatua hizo, alisema zinakwenda sambamba na uwekezaji mkubwa katika usafiri na usafirishaji nishati ya umeme, kilimo cha uhakika na viwanda.

"Nyote mtakubaliana nami kwamba ufanisi wa huduma hizi kwa kiasi kikubwa unaathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira ambao kwa takribani asilimia 95 ni matokeo ya shughuli za kibinadamu," alisema.

Majaliwa alisema Tanzania ni moja ya nchi zinazoathiriwa na changamoto za uharibifu wa mazingira unaosababisha mabadiliko ya tabianchi kupitia shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwamo uvamizi wa maeneo tengefu, vyanzo vya maji na matumizi holela ya mbolea zenye kemikali na viuatilifu; ufugaji wa kuhamahama unaojumuisha makundi makubwa ya mifugo na ukataji holela wa miti kwa ajili ya kuni.

Shughuli zingine, alisema ni uchomaji wa mkaa na upanuzi wa mashamba na makazi; uchomaji moto ovyo wa misitu na mbuga, uchimbaji wa madini usio endelevu na uvuvi haramu, uvunaji haramu wa mikoko na kuenea kwa viumbe vamizi.

# Wasiojulikana wavamia msikiti, waua mlinzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU wasiofahamika wamevamia msikiti wa Shree Hindu Mandal Temple na kumuua mlinzi, Bakari Kasarani (46), mkazi wa wilaya ya Kahama.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema lilitokea usiku wa kuamkia Machi 30, mwaka huu, huku akilaani mauaji hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mndeme aliyefika eneo la tukio alisema mlinzi huyo alikuwa ni wa kampuni binafsi, kwamba serikali itahakikisha waliotekeleza tukio hilo wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mndeme ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alisema serikali itagharamia uharibifu uliofanywa ndani ya msikiti huo, huku akimtaka msimamizi wa msikiti huo kuzijulisha mamlaka ili kusaidia kurejesha hali ya msikiti huo ili waumini waendelee na ibada zao.

"Tumesikitishwa sana na tukio hili, tunatoa pole kwa waumini pamoja na viongozi wa msikiti huu, waliohusika na tukio hili tutawasaka popote walipo na tutahakikisha wanakamatwa na wanachukuliwa hatua za sheria," alisema Mndeme.

Ilielezwa kuwa watu hao baada ya kutekeleza mauaji hayo waliingia msikitini na kuiba vito vya thamani sambamba na kuvuruga vitu vyote vya ibada vilivyokuwemo katika msikiti huo. Akizungumzia tukio hilo jana, msimamizi wa msikiti huo, Niraj Kakad, alisema walipokea taarifa hizo kutoka kwa mwenyekiti wao na kuchukua hatua za haraka kuanza kufuatilia na kubaini kuwa watu hao walivunja na kuiba vito vya thamani vya kufanyia ibada na sadaka iliyokuwa msikitini.

"Thamani ya vitu hivyo sitaweza kuibainisha lakini ni vitu vya ibada pamoja na sadaka zilizokuwepo msikitini," alisema Kakad. Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, aliiomba serikali kufanya uchunguzi wa kina wa tukio hilo na kuhakikisha wahusika wote wanakamatwa ili kudhibiti vitendo hivyo katika Mkoa wa Shinyanga.



Mwonekano wa kituo cha mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), wakati ujenzi ukiendelea katika barabara ya Kilwa, Kurasini, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Othman ataka mfungo Ramadhani kuwa elimu katika kutenda mema

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni vyema kwa viongozi wenye dhamana katika nafasi mbalimbali, kuyafanyia kazi kwa vitendo mafunzo ya imani na nidhamu wanayoyapata katika Mwezi Mtukufu.

Amesema kwa kufanya hivyo, kutaiwezesha Zanzibar kuepukana na masuala mbalimbali yanayoirejesha nyuma kwa kuamini kwamba Mwenyezi Mungu yupo wakati wote.

Othman ameyasema hayo juzi katika Ukumbi wa Shekhe, Idrisa Abdulwakili, Kikwajuni, mjini Zanzibar alipowasalimia viongozi na wananchi mbalimbali baada ya kukamilika kwa futari ya pamoja iliyoandaliwa na ofisi yake.

Alisema mikusanyiko ya ibada ikiwamo futari ya pamoja wanayokaa wananchi na waumini mbalimbali, inasaidia kuvunja na kuondosha mambo yanayotenganisha wananchi na kuongeza chuki miongoni mwao na kwamba hali hiyo ndiyo msingi wa kuwa pamoja na kudumisha umoja na mshikamano. Kwa mujibu wa Othman, mikusanyiko ya namna hiyo ni muhimu na inatoa fadhila nyingi za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa kumwomba Mwenyezi Mungu msamaha kwa yale mtu aliyokosa.

Alisisitiza kwamba ni wajibu wa waumini kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwakumbusha wananchi na waumini wa Kiislamu kwamba mbali ya fadhila za ramadhani zilizowekwa na Mungu, ni chuo muhimu cha elimu ya kujenga nidhamu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Suala la kujenga nidhamu miongoni mwa waumini na wananchi, alisema linasaidia taifa kupiga hatua na kupata maendeleo na kamwe hakuna mwananchi au kiongozi anayeweza kufanikiwa kwa lolote bila kufuata nidhamu. Alisema Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unatoa funzo kubwa kwa jambo hilo sambamba na umuhimu wa kumcha Mungu na kutegemea malipo yake.

Othman alisema kufunga Ramadhani kwa waumini ni kutekeleza kwa vitendo elimu ya nidhamu katika kiwango cha juu cha mafunzo yatokanayo na funga hiyo na kusisitiza waumini hao kuendeleza mambo yote mazuri hata baada ya mfungo.

Pia alisema ni vyema Waislamu wote kuiendeleza nidhamu inayopatikana katika mwezi mzima wa Ramadhani ili wananchi na Waislamu kwa jumla, waonyeshe kuhitimu kwao mafunzo yaliyopatikana katika kipindi hicho na elimu hiyo iwe na manufaa zaidi duniani na ahera.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Mgharib, Idrisa Kitwana Mustafa akitoa salamu za mkoa baada ya futari hiyo, aliitaka jamii kukemea maovu yaliyomo ndani ya maeneo yao hasa suala la kuwepo madanguro na upigaji wa muziki bila kufuata taratibu.

Alisema vitendo hivyo ni kichocheo cha maovu mengi kutokea na vinasababisha kero kubwa kwa wananchi na waumini. Kitwana aliwataka wananchi kushikamana na kupendana kwa wema na kukumbushana katika mema na kuachana na mabaya. Pia aliwaomba wananchi wote kukemea vitendo vya ushoga ambavyo vimekuwa vikishamiri kutokana na kuhamasishwa sehemu nyingi duniani.

## ... Mtoto afariki dunia kutumbukia katika shimo la maji

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MTOTO Robert Maganga (2), mkazi wa Kijiji cha Ngogwa Manispaa ya Kahama amefariki dunia huku mwenzake akiwa katika hali mbaya baada ya kutumbukia katika shimo la kuvuna maji lililokuwa nyumbani kwao.

Baba wa mtoto huyo, Gabriel Robert, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 2:00 asubuhi wakati alipokwenda kumhudumia mteja wake wa mihogo shambani.

Alisema mtoto wake alikuwa akimfuata mama yake aliyekuwa akivuna mahindi shambani ambako kuna bwawa lililochimbwa miaka 10 iliyopita kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

"Walikuwa wameongozana na wenzake wawili, mmoja wa miaka miwili na nusu na mwingine miaka mitatu. Walishindwa kuvuka eneo hilo ndipo wawili wakatumbukia katika shimo hilo la maji," alisema Robert.

Alisema kati ya watoto hao ni mmoja tu wa miaka mitatu ambaye hakutumbukia kwenye bwawa hilo na kukimbia kuwaita ndugu baada ya kuona wenzake wamezama.

Pia alisema baada ya kuwatoa katika shimo hilo walikimbizwa katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama lakini Maganga alifariki dunia kabla ya kufika hospitalini, huku mtoto mwingine akiendelea na matibabu.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Sophia Shabani, alikiri kuwapokea watoto hao, kusema mmoja amelezwa na anaendelea na kupatiwa matibabu na mwingine alifikishwa akiwa ameshafariki.

Diwani wa Kata ya Ngogwa, Kamuli Mayunga, alisema watoto wanatakiwa kupata ulinzi, aliwashauri wananchi wote wenye mabwawa au mashimo karibu na nyumba zao kuyawekea uzio ili kuepusha vifo visivyo vya lazima kwa watoto wadogo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Leonard Nyandahu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.



Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Mtinika ( katikati), Mwenyekiti wa Taasisi ya Umoja na Amani Kwanza, Idrissa Kaneka (kulia) na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Prosper Mutalemwa, wakishiriki ufyekaji wa kichaka kilichokuwa kikitumika kufanyia uhalifu eneo la Mzinga Darajani, Mbagala, Dar es Salaam jana.
**PICHA: IMANI NATHANIEL**

# RAS awaangukia walimu mapambano ushoga

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, amewataka walimu kusaidia kupambana na tatizo la mapenzi ya jinsia moja (ushoga) na usagaji shuleni kwa kuwa wao ni walezi wa wanafunzi kuanzia ngazi ya chekechea hadi elimu ya juu.

Akizungumza juzi wakati akifungua kikao cha Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari (TAHOSSA) Mkoa wa Singida, Dk. Mganga alisema sasa hivi kumekuwa na tatizo kubwa la ushoga, hivyo zinatakiwa jitihada za dhati katika kunusuru wanafunzi kujiingiza kwenye vitendo hivyo ambavyo ni kinyume cha utamaduni wa kitanzania.

Alisema walimu wanaweza kuzuia watoto kujiingiza katika vitendo hivyo kwa kuwa jirani na watoto hao na kufuatilia mienendo yao kwa kushirikiana na wazazi wao.

"Wote tuliona Dk. Harrison Mwakyembe (mbunge na waziri wa zamani) wakati akizungumzia suala la ushoga ambalo walengwa zaidi wanaotafutwa kujiingiza katika vitendo hivyo ni vijana wadogo, hivyo walimu chukueni hatua kuwanusuru wanafunzi na janga hilo," alisema.

Kuhusu taaluma alisema walimu wakiamua wanafunzi wote watafaulu na kuondoa kabisa alama ziro na kuwaomba walimu kujenga ushirikiano na wazazi na walezi ili kujua changamoto za watoto wakiwa shuleni na nyumbani jambo litakalosaidia kuwaweka sawa.

Dk. Mganga alisema changamoto za watoto darasani haziwezi kuwa za wazazi, mila au desturi bali ni za walimu na akahoji inakuweje watoto asilimia 90 darasani wote wapate alama F.

"Walimu wa enzi zetu wanafunzi walipokuwa wakifanya vibaya katika mitihani yao walikuwa wakiumia sana na ninyi ebu igine hilo kwa ajili ya kuwasaidia watoto" alisema Mganga.

Mganga aliwaomba walimu hao waende wakakomae na hawatashindwa na kupitia wao hakuna litakaloshindikana kwani Serikali inawategemea.

Aliwataka walimu waende kutoa faraja katika familia, waende kutengeneza wasomi, wakafanye kazi kwa uzalendo kwa kuwainua watoto hao kitaaluma na kuwa watapata baraka kutoka kwa wazazi na Mungu.

Mganga alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kujenga miundombinu ya madarasa ili wanafunzi wapate maeneo mazuri ya kusomea ambapo kwa Mkoa wa Singida madarasa 620 yenye thamani ya Sh. bilioni 12.4 yamejengwa, hivyo njia pekee ya kuheshimisha ni kufaulisha wanafunzi wote na asiwepo wa kupata daraja la tatu wala ziro bali wapate daraja la kwanza na la pili.

Aidha, Mganga aliwataka walimu hao kuwashirikisha wazazi kukarabati samani za shule zinazoharibika ambazo zimekuwa zikiwekwa katika moja ya madarasa badala ya kusubiri serikali ifanye kazi hiyo.

Akizungumzia suala la chakula kwa wanafunzi, aliwataka walimu hao kila shule kuwa na mashamba kwa ajili ya kulima mahindi na mazao mengine na akahimiza suala zima la utunzaji wa mazingira ya shule kwa kupanda miti na maua na wanafunzi wawe na vidumu vya maji kwa ajili ya kumwagilia.

"Kuanzia mwaka ujao tutaanza kufanya mashindano ya utunzaji wa mazingira na shule itakayoshinda tutaipatia zawadi" alisema Mganga.

Mganga pia aliwataka walimu hao kwenda kuanzisha elimu ya kujitegemea katika shule zao kwa kufuga, mbuzi, ng'ombe, kuku na kufungua miradi midogo midogo ambayo itawapatia kipato na kuwajengea uwezo wanafunzi wa kujua mbinu za kujitegemea kuanzia wakiwa shuleni.

Dk. Mganga aliwahimiza walimu hao kufanya kazi kwa bidii na kujituma na kuwa adui yake mkubwa ni mtumishi yeyote ambaye atashindwa kufanya hivyo na kuwa hata mvumilia hata kidogo.

Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Dk. Elpidius Baganda, alisema kazi kubwa wanayotarajia kuifanya ni kupita mashuleni kwa siku sita kila wiki kwa ajili ya kuangalia kama tathmini za mitihani ya kidato cha nne na tatu zilizochukuliwa ni sahihi.

Alisema jambo lingine watakalolitilia kipaumbele ni suala zima la upatikanaji wa chakula mashuleni sambamba na kuangalia miradi mbalimbali ambayo Serikali imetoa fedha nyingi kama imekamilika kwa asilimia 100.

Mwenyekiti wa TAHOSSA, Paschal Kichambati, alisema changamoto zao nyingi huwa zinatatuliwa kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa hadi taifa na kuwa TAHOSSA kazi yake kubwa ni kuleta utulivu.

Kuhusu miradi inayofanyika mashuleni chini ya usimamizi wa walimu hao alisema licha ya kuwa ni walimu wamekuwa wahandisi wabobezi kwa kuweza kuisimamia na kukamilika kwa ubora na kwa kiwango cha hali ya juu na kwa thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali.

Alisema baadhi ya walimu kwenye akaunti zao za shule wamekuwa na fedha kuanzia Sh. milioni 30 hadi 80 kwa ajili ya kumalizia miradi hiyo na wamekuwa wazalendo na waaminifu katika matumizi ya fedha hizo.

# Mpango kuzindua mchakato Dira ya Taifa ya Maendeleo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, kesho anatarajiwa kuzindua mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo itatoa maono na kuweka malengo ambayo taifa linataka kuyafikia ndani ya kipindi cha miaka 25 ijayo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Jenifer Omolo, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa kuhusu uzinduzi wa mchakato huo kwa waandishi wa habari ambao unatarajiwa kufanyika jijini hapo.

"Dira hii itatoa maono na kuweka malengo ambayo taifa letu linataka kuyafikia ndani ya kipindi cha miaka 25 ijayo baada ya kuisha kwa kipindi cha utekelezaji wa Dira tuliyo nayo sasa ya Taifa ya Maendeleo 2025.

"Maandalizi ya Dira mpya ya 2050 yanakidhi matakwa

ya Katiba ambayo ndio mwongozo mkuu wa nchi yetu," alisema Omolo.

Aidha, alisema mwaka 2009/10, serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025 kupitia mikakati na programu za maendeleo. Alisema tathmini hiyo ilibainisha uhitaji wa Taifa kuanza kupanga vipaumbele vya nchi.

"Suala hili lilipelekea kuandaliwa kwa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP) 2011/12 - 2025/26)," alisema Omolo. Na kuongeza kuwa mpango huo wa miaka 15 ulipangwa kutekelezwa kwa mipango ya muda wa kati ya miaka mitano na mipango ya muda mfupi ya mwaka mmoja.

"Katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, taifa limepiga hatua kubwa ya maendeleo katika nyanja mbalimbali hususan za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

"Hata hivyo, utekelezaji wa Dira 2025 unafikia tamati mwaka 2025. Kwa msingi huo, ni jukumu letu sote kwa nafasi zetu kuanza kufikiria juu ya mafanikio ya utekelezaji wa dira 2025 na mustakabali wa nchi yetu katika miaka ya mbele ijayo," alisema.

Kadhalika, alisema ili kufanikisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kunategemea kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wadau wote.

"Hivyo, nitoe rai kwa wadau wote katika maeneo yao kushiriki kikamilifu katika kutoa mchango wao utakaowezesha kuandaliwa kwa Dira yenye maono ya watanzania kwa miaka 25 ijayo," alisisitiza Omolo.

## HABARI KITAIFA

# Mchakato kuhamisha makaburi kupisha ujenzi SGR waiva

**Na Halfani Chusi**

MCHAKATO wa uhamishaji makaburi kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) mkoani Tabora unaelekea kukamilika.

Hayo yalisemwa mapema wiki hii na na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Manyoni, Ahmed Makele, wakati wa kikao cha viongozi na wananchi wa wilaya ya Manyoni.

Kamanda Ahmed alitoa wito kwa serikali ya kijiji na ndugu wa marehemu kuendelea kutoa ushirikano ili kuhakikisha mchakato huo unaenda salama.

Alisema TRC imefanya jambo la msingi kwa kuanza kutoa elimu kwa wafiwa juu ya utaratibu utakao tumika kuhamisha makaburi hayo, akisisitiza kuwa hatua hiyo itaondoa migogoro kati ya serikali na wananchi.

"Nitoe wito kwa viongozi na wananchi waendelee kutoa ushirikiano katika mchakato huu na hatimaye kazi iendelee" alisema.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Majengo, Hassan Simba, alisema yeye na viongozi wenzake watatoa ushirikiano kwa TRC na mkandarasi wake kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa.

"Reli hii ikikamilika itarahisisha shughuli za kijamii na kilimo kwa wakazi wa Manyoni pamoja na kuongeza kipato kwa kuwa watu watatumia usafiri huo kupeleka bidhaa sehemu mbalimbali," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wa dini walioshiriki mchakato huo, Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Itigi, Chiristopher Kiwango, aliishukuru TRC na uongozi wa wilaya kwa kuzingatia haki za binadamu, sheria na misingi ya imani wakati wa kuhamisha makaburi.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupa viongozi waliosimamia mchakato huu ambao umefanyika kwa utaratibu uliozingatia mambo ya afya, imani za marehemu pamoja na haki za binadamu, hivyo tunamshukuru Mungu lakini pia shukrani ziende kwa wale wote walioshiriki katika kazi ya kuhamisha makaburi," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bosphorus inayotengeneza bidhaa zinazozuia unyevu katika kuta za majengo, Necmetin Keles (kulia), akionyesha bidhaa zinazozalishwa na kampuni hiyo zijulikanazo kwa jina la Yapfix Wall Putty katika kiwanda hicho kilichoko Boko, Dar es Salaam, juzi. Kushoto ni Meneja wa Kiwanda hicho, Ale Alex. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MOI yafanya upasuaji watoto vichwa vikubwa

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), imefanya upasuaji kwa watoto wawili wenye vichwa vikubwa, kupitia kambi maalum ya matibabu ya kibingwa na bobezi inayoendeshwa na madaktari bingwa.

Taarifa iliyotolewa na MOI jana ilisema upasuaji huo ulifanywa na madaktari bingwa kutoka MOI kwa kushirikiana na wataalam wa Hospitali ya Rufani ya Nkinga, mkoani Tabora.

Daktari Bingwa wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu kutoka MOI, Dk. Alpha King'omela, akizungumzia huduma hiyo mkoani Tabora, alisema lengo la kambi hiyo ni kuendelea kuwajengea uzoefu madaktari, wauguzi na wataalam walioko katika Hospitali ya Rufani Nkinga, Tabora.

"Hospitali ya Rufani Nkinga ina wataalamu wenye uwezo mkubwa na vifaa vya kutosha vya kufanyia upasuaji wa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, ndiyo maana tumefanikiwa kuwafanyia huo upasuaji," alisema Dk. King'omela.

Daktari wa Upasuaji wa Hospitali ya Rufani ya Nkinga, Dk. Richard John, aliwashukuru wataalam wa MOI kwa kuwajengea uwezo huo.

"Kwa mara ya kwanza, nimeshiriki kuwafanyia upasuaji watoto wawili wenye vichwa vikubwa katika hospitali yetu. Awali watoto hawa tulikuwa tunawapa rufaa (rufani) ya kwenda kutibiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando na MOI lakini sasa tumejengewa uwezo na upasuaji huu utakuwa unafanyika hapa kwetu," alisema Dk. John.

Mmoja wa wazazi walipeleka watoto kufanyiwa upasuaji (jina limehifadhiwa) alisema amenufaika kwa mtoto wake kufanyiwa upasuaji kupitia kambi hiyo kwa sababu afya ya mtoto wake kwa sasa inazidi kuimarika.

Alisema awali mtoto wake alikuwa ana changamoto nyingi lakini sasa anaendelea vizuri baada ya upasuaji.

MOI inazidi kutekeleza kwa vitendo agizo la serikali kuzidi kuongeza wigo mpana wa tiba za kibingwa na bobezi katika hospitali za rufaa na mikoa.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAFRONIA BLASTO MAKUNDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC817CWE**.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/115981/2023**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ALLY RAJABU BORI** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE422397 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 17/09/2021.Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DAR/KIG/RB/415661/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HARALD PHILEMON LUAMBANO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 790 DKS - MASSEY FERGUSON.** Chassis No. **R379030.** Engine No. **7903056**.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/116302/2023.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF IRAMBA**
**AT KIOMBOI**
**CIVIL CASE NO. 02 OF 2023**
**KERPHAS SAMSON..............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**SUNCHINE MINING LIMITED..........DEFENDANT**
**SUMMONS TO APPEAR**
**TO: SUNSHINE MINING LIMITED**
**C/O**

You are hereby commanded/ordered in the name of the United Republic of Tanzania to attend this court on the 04th day of April, 2023 at 08:00 am in the above case and not to depart without leave of the court and you are hereby warned that if you shall without just excuse, neglect to obey this summons a warrant will be issued to compel your attendance, and you will furthermore render yourself liable to a fine as shall be determined by the Court.

**GIVEN** under my hand and the SEAL of the Court this 23rd day of March, 2023.

This summons has been issued on the application of JUDICIARY.

MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
KIOMBOI - IRAMBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 179 YA 2022**
**(**kutoka kwenye madai kesi na 234/2022**)**
**WILLIAM MALLECELA @ LE MUTUZ........ MDAI**
**DHIDI YA**
**PATRICK CHRISTOPHER KAMWELWE..... MDAIWA**
**KWA:**
**PATRICK CHRISTOPHER KAMWELWE.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii nyie binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe **03/04/2023 saa 7:00 mchana** mbele ya **Mhe. R.E Kabate - HAkimu Mkazi Mkuu.** Kwa majibu ya madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima ulete nyaraka zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya utetezi wako.

**ANGALIZO:**

Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 06 mwezi wa Machi, 2023

R. E. KABATE
HAKIMU MKAZI MKUU
DAR ES SALAAM – KISUTU.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NG'ARAGA JACKSON NGARAGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 395 BYX - MITSUBISHI CANTER**. Chassis No. **FE562EV540291**. Engine No. **4M51A13759**.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/115666/2023**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Rais kuhusu mashirika mizigo litekelezwe kwa haraka

**WIKI** hii, Rais Samia Suluhu Hassan alipokea ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Katika ripoti ya CAG iliyofanya ukaguzi katika wizara, idara na taasisi za serikali, pamoja na mambo mengine, imeibua kuwapo kwa mashirika ya umma ambayo yamekuwa mzigo kwa serikali kutokana na kufanya kazi kwa hasara kila mwaka. Miongoni mwa mashirika hayo ni Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Baada ya kupokea taarifa hizo, Rais Dk. Samia alisema mashirika hayo yamekuwa yakipatiwa fedha kila mwaka kutoka serikali kuu kwa ajili ya uendeshaji na yamekuwa yakishindwa kutoa faida na hata gawio kama sheria inavyotaka. Kutokana na serikali kupeleka fedha kila mwaka, mashirika hayo yamekuwa mzigo, hivyo kuna kila sababu ya kufanya tathmini ya uwapo wao na yale yanayoonekana hayana tija yafutwe kabisa.

Katika kusisitiza hilo, Rais alisema NDC katika miaka mingi imeshindwa kufanya kazi zake ipasavyo ilhali imekuwa ikipatiwa mabilioni ya fedha kwa ajili ya maendeleo. Bila kupindisha maneno, Rais Samia alisema shirika hilo limekuwapo tangu alipokuwa akisoma shule, hivyo inakuwa ngumu kwake kuamini kama madhumuni ya kuanzishwa kwake bado yana mashiko.

Licha ya NDC, alisema TTCL imeshindwa kabisa kufanya biashara ya mawasiliano ya simu, hivyo kama inawezekana iache shughuli hiyo ibaki na uendeshaji wa mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Shirika hili lilianzishwa mwaka 1994 baada ya kugawanywa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania, hivyo kuzaliwa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na Shirika la Posta Tanzania (TPC). Aidha, ikumbukwe kwamba shirika hilo lilibinafsishwa mwaka 2000 kabla ya kurejeshwa serikalini miaka ya karibuni baada ya kuwapo sintofahamu za kimkataba pamoja na uendeshaji.


Ni kweli kwamba yako mashirika mengi yaliyo chini ya serikali ambayo yamekuwa mzigo kutokana na kuzalisha hasara kila mwaka kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kiushindani kutoka kampuni za kibiashara zinazofanya kazi zinazofanana na zile zinazofanywa na mashirika hayo. Lakini pia uendeshaji wa mashirika hayo ni chanzo cha kudorora kutokana na baadhi kutokuwa na sifa na uwezo katika kusimamia taasisi hizo.

Kama alivyosema Rais, wakati umefika wa kuyafanyia tathmini mashirika hayo ili kupata picha halisi kama yanastahili kuwapo au la. Ni imani kwamba agizo lililotolewa na Rais Samia kwa Katibu Mkuu Kiongozi pamoja na wasaidizi wake yatafanyiwa kazi haraka ili kunusuru fedha za umma ambazo zimekuwa zikipotea kwa ajili ya kupatiwa mashirika hayo.

Pamoja na serikali kufanyia kazi suala hilo, ni vyema pia ikafahamika kwamba kwa takriban miaka 30 sasa, Tanzania iliingia katika uchumi wa soko ambao unaruhusu ushindani tofauti na uchumi hodhi uliokuwapo tangu kuanzishwa kwa Azimio la Arusha. Kwa mantiki hiyo, serikali inapaswa kujielekeza katika jukumu lake la kuwa mwezeshaji kwa kuweka mazingira sawa ya ushindani na kuweka sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya ushindani badala ya kuwa mshiriki katika ushindani.

Kwa ujumla, ni vyema serikali ikawa mdhibiti badala ya kumiliki taasisi za kibiashara, hivyo kuiachia sekta binafsi katika masuala mbalimbali kwa kuwa katika muktadha wa uchumi wa soko, sekta binafsi ndiyo kitovu cha ukuaji wa uchumi. Kupitia ukuaji na maenedeleo ya sekta binafsi, serikali itapata fedha zitokanazo na kodi mbalimbali, hivyo kupata uwezo wa kujiendesha kibajeti pamoja na kuepukana na mzigo wa mashirika yasiyo na tija.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kilio cha wadau kwa ndoa za utotoni kisikike



Na Sabato Kasika

**UMRI** wa mtoto wa kike kuolewa, limekuwa miongoni mwa mambo yanayojadiliwa kwa muda mrefu na watu wa kada mbalimbali katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, huku kukiwa na maoni yanayopingana.

Wako baadhi ya watu ambao wanataka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 11 hadi 13 ambaye amevunja ungo, aruhusiwe kuolewa kwa amri ya mahakama, kwa kuzingatia vielelezo vya kimazingira ikiwamo afya.

Katika umri huo, imani, mila na desturi za jamii husika vizingatiwe, ingawa inawezekana mhusika akawa na madhara kiafya pale anapopata ujauzito na kujifungua, kwani viungo vyake vya uzazi havijakomaa.

Lakini pia wapo wengine ambao wanapendekeza Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ifanyiwe marekebisho hasa katika vifungu vya 13 na 17 kwa madai kwamba vinaruhusu mtoto wa miaka 15 aolewe kwa ridhaa ya wazazi.

Pamoja na hayo, ninaamini kwamba ndoa za utotoni ni tatizo kwani zinaweza kusababisha watoto wa kike kushindwa kutimiza ndoto zao katika elimu, hali duni za maisha na madhara ya kiafya kwa mabinti.

**Pamoja na hayo, ninaamini kwamba ndoa za utotoni ni tatizo kwani zinaweza kusababisha watoto wa kike kushindwa kutimiza ndoto zao katika elimu, hali duni za maisha na madhara ya kiafya kwa mabinti.**

Ndoa kwa mabinti wa umri mdogo zimekuwa zikitajwa kama mateso, ambayo wadau wa kutetea haki za binadamu, wakiwamo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), wanatamani umri wa kuolewa uanzie miaka 18.

Wanaamini kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inapingana na sheria nyingine ikiwamo ya mtoto inayomtaka kutojihusisha na vitendo vya ngono hadi atakapofikisha umri wa miaka 18.

LHRC pia inagusia Sheria ya Kanuni ya Adhabu inayotambua kosa la kufanya mapenzi na mtoto chini ya miaka 18 pamoja na Sheria ya mikataba inayotambua umri wa kuingia mikataba ni miaka 18.

Wanazingatia Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inayotoa ufafanuzi kuwa mtoto ni mtu aliye na umri chini ya miaka 18, na kwamba kuanzia miaka 18 kwenda juu ni mtu mzima ambaye ana uwezo wa kuamua jambo.

Kimsingi pamoja na hayo yote, nguzo muhimu ya kutokomeza ndoa za utotoni, ni kuweka mfumo imara wa sheria unaoweka umri wenye uwiano wa kuolewa au kuoa makundi hayo ya jinsi mbili kuwa miaka 18.

Ninaamini kwamba hatua zikichukuliwa za kuwekwa umri ambao umekuwa ukitajwa na wadau wa kutetea haki za binadamu, hakutakuwa na ndoa za utotoni na pia watoto wa kike wanaweza kuwa salama zaidi.

Watakuwa salama kwa sababu wanaweza kuepuka kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI, magonjwa ya zinaa, manyanyaso, athari za kisaikolojia, kimwili na ukatili wa kijinsia kupitia ndoa hizo za utotoni.

Utafiti wa Demografia ya Afya Tanzania (TDHS) uliowahi kufanywa nchini, ulionyesha kuwa ndoa za utotoni ziko zaidi vijijini, lakini kwa mijini zikishamiri kwa familia maskini na zenye imani kali za kidini na kimila.

Vilevile, utafiti huo ukaonyesha kuwa wasichana kutoka familia zenye kipato cha chini, wana uwezekano mkubwa wa kuolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 kuliko wasichana wanaotoka katika familia za kipato cha juu.

Sasa ni wazi kila mmoja anahusika katika vita dhidi ya ndoa hizo. Watunga sheria waitazame upya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, jamii nayo iachane na kigezo cha umaskini, mila na desturi kufanya ukatili huo wa kijinsia.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# CAG apewe meno ang'ate ili madudu yasijirudie tena



Pascal Mayalla

SISI wanahabari na vyombo vya habari, tuna wajibu na jukumu la kuisaidia nchi, serikali, viongozi na taasisi zake ikiwamo mihimili ya Serikali, Bunge na Mahakama. Inapotokea kuna mahali panalegalega, ni wajibu wa vyombo vya habari kupasema ili kuisaidia serikali yetu na nchi yetu.

Siku za nyuma, niliwahi kusema kitu kuhusu mhimili wa Bunge. Kutokana na kuusema mhimili huo, mimi na mhariri wa gazeti lile tukaitwa kuhojiwa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge. Leo katika makala hii, najitahidi sana kutumia lugha nzuri na ya staha ili kulinda kibarua changu na mhariri wangu lakini wajibu wa vyombo vya habari wa kuihudumia jamii na kulisaidia taifa ni wajibu mkubwa zaidi kuliko kulinda kibarua.

Ukiona taasisi inachachamaa sana inapokosolewa, ujue tuhuma hizo ni kweli. Tanzania tumepata uhuru kutoka kwa Waingereza, hivyo uendeshaji wa serikali yetu pia tumeiga na kutumia mfumo wa Uingereza uitwao 'Westminster System" ambao ni mfumo wa Kiingereza.

Nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa katiba, sheria, taratibu na kanuni kupitia mihimili ya Serikali, Bunge na Mahakama ikisaidiwa na taasisi kadhaa zinazojitegemea ambazo ama zinawajibika kwa serikali au Bunge. Moja ya taasisi zinazojitegemea na kuwajibika kwa Bunge ni ofisi ya CAG.

Mihimili yote mitatu, kila mmoja unatimiza majukumu yake kwa mamlaka yake yenye uhuru bila kuingiliwa. Kwa lugha ya Kiingereza inaitwa "Independence Powers". Bunge kazi yake ni kutunga sheria na kuisimamia serikali. Mahakama kazi yake ni kutafsiri sheria zilizotungwa na Bunge na utoaji wa haki ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na serikali kazi yake ni kutekeleza sheria zilizotungwa na Bunge na uamuzi wa Mahakama.

Katika utekelezaji wa majukumu ya mihimili hii yote mitatu, kila mhimili una uhuru wake wa kutoingiliwa na una wajibu wa kuwa mlinzi wa mhimili mwingine (watchdog) ili mhimili mmoja usikiuke mamlaka yake kupitia kanuni inayoitwa "The Principal of Separation of Powers, Checks and Balance".

Lengo la Waingereza kuweka mfumo huu wa 'checks and balance' ni kuhakikisha kila mhimili unatimiza wajibu wake huku ukijijua kuna mtu ananiangalia, hivyo lazima awajibike na asipowajibika anaangaliwa na mhimili mwingine.

Serikali ya 'Westminster System' yenye mfumo wa 'parliamentary supremacy' chini ya Waziri Mkuu Julius Kambarage Nyerere, ilidumu kwa mwaka mmoja tu toka Desemba 9, 1961 mpaka Desemba 9, 1962 tukawa Jamhuri ambao ni mfumo wa Kimarekani wa kuwa na Rais, hivyo Rais wa nchi ndio kila kitu. Kuanzia mwaka 1965 tulifuta vyama vingi na Tanzania kuwa ni nchi ya chama kimoja na kuanzisha mfumo mpya wa Kitanzania wa kutawala nchi, mfumo wa Chama kushika hatamu kuongoza serikali uitwao "Party Supremacy". Kupitia mfumo huo, chama ndiyo kila kitu, na si Bunge, si serikali.

Kutokana na mfumo huu, zile 'checks na balances' zilisimamiwa na chama kwa Bunge la chama kimoja, serikali ya chama kimoja, mahakama ikawa tawi la chama na hata majeshi pia yalikuwa tawi la chama.

Tulipopitisha Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, ilikuwa katiba ya mfumo wa chama kimoja huku chama ndicho chenye hatamu za kuongoza serikali. Mwaka 1992, tuliporejea kwenye mfumo wa vyama vingi, ilitubidi tubadili katiba na kuwa na katiba mpya ya vyama vingi. Hata hivyo, lakini tuliingia mfumo wa vyama vingi kwa kuiwekea viraka katiba ya chama kimoja kuigeuza kuwa ya vyama vingi bila kurudisha mamlaka ya Bunge kwa wananchi. Japo sasa tuna mfumo wa 'parliamentary supremacy', bado chama ndicho kila kitu.

Japo chama hakishiki hatamu kikatiba, kiutendaji japo Rais ndiye mkuu wa nchi, mkuu wa serikali, na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na wakati huo huo ndiye mwenyekiti wa chama tawala na Spika wa Bunge ambaye ni Mkuu wa Mhimili wa Bunge ni mjumbe wa Kamati Kuu ya chama tawala.

Ili mtu kugombea nafasi yoyote ya uongozi ni lazima updenekezwe na chama cha siasa na ukifutwa uanachama unapoteza uongozi, hivyo bado chama ndiyo kila kitu! Kutokana na wakuu wa mihimili kuheshimiana, Bunge ndilo lenye jukumu la kuisimamia serikali. Hebu tuelezane ukweli, iwapo serikali itafanya makosa kama yanavyojirudia kwenye ripoti ya CAG, Bunge la CCM linaloongozwa na Spika ambaye ni mjumbe tu wa Kamati Kuu ya CCM, anaweza kusimamia serikali ya Rais wa JMT ambaye ni mwenyekiti wake? Mfumo huo wa wazungu Waingereza ulianzisha baadhi ya ofisi za kujitegemea zinazoiangalia serikali lakini zinawajibika kwa Bunge. Moja ya ofisi hizi ni ofisi ya CAG. Kwa miaka kadhaa sasa, ripoti ya CAG imekuwa ikionyesha madudu ya serikali yakijiridia mwaka hadi mwaka.

Bunge ambalo ndilo msimamizi wa serikali, lilipaswa kuhakikisha hoja za CAG zinajibiwa kikamilifu na mapendekezo ya CAG na kuhakikisha madudu ya ripoti moja hayajirudii. Lakini kinachotokea kwenye ripoti ya CAG ni madudu kujirudia mwaka hadi mwaka. Hii maana yake kuna mtu hatimizi wajibu wake kikamilifu wa kuisimamia serikali! Kama msimamizi huyo ameshindwa kuisimamia serikali, nashauri kwa kuuliza, je tutunge sheria CAG apewe meno ang'ate? Kinachofanya CAG asiwe na meno ni ile ile kanuni ya 'separation of powers', CAG akague tu na kutoa mapendekezo kwa Bunge, msimamizi wa serikali. Sasa inapotokea msimamizi kushindwa kusimamia, madudu yanajirudia, kuna ubaya CAG naye akipewa meno, akaundiwa 'CAG Quasi Judicial body' na kuwatundika 'msalabani' hao wafanya madudu ili kukomesha na yasijirudie?

Kama mamlaka nyingine zote za udhibiti zina vyombo vya kisheria zikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (SUMATRA), Mabaraza ya Ardhi pamoja na Kamati ya Kinga na Nadaraka ya Bunge, nini kinashindikana kwa CAG kupewa meno ang'ate?

**Wasalaam**
**Paskali 0754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Uchuuzi tuufanyao mitaani ni halali?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WACHUUZI wa Sheba na wa Rama walifanya biashara nawe, walikuletea viungo vya chakula, vito vya thamani na dhahabu na kujipatia bidhaa zako safi."

Ni nukuu kutoka kitabu cha Ezekieli 27:22-36 kwenye Biblia, kinachothibitisha historia ya wachuuzi katika jamii zetu waliotafuta bidhaa na kuziuza kwa kubadilishana kwa kutokuwapo fedha enzi hizo.

Wachuuzi walikuwa watu muhimu kwa maisha ya jamii kwani walirahisisha upatikanaji wa bidhaa, lakini pia walipunguza gharama na muda wa kusafiri kuzifuata. Walikuwapo na hata sasa wapo.

Serikali yetu kwa nia njema, imekuwa ikiwakumbatia wachuuzi wengi wao wakiwa vijana masikini, wanaojipatia faida ndogo, fedha zao zikiwa ni za bora mkono uende kinywani.

Wamekuwa msaada mkubwa kwa jamii, kwa kurahisisha kupata bidhaa kwa bei nafuu ya majadiliano lakini pia kupunguza msongamano katika masoko na maduka ya vyakula.

Utawasikia mitaani wakiuza mboga mboga, matunda na kadhalika. Ili mradi bidhaa zikiuzwa mitaani huku wauza 'bangili' wakiuza bangi.

Hiyo maana yake ni kwamba miongoni mwa wachuuzi kuna wasio waaminifu kwa maana ya mbweha waliojifunika ngozi za kondoo.

Hivi sasa katika kila kona ya nchi, kuna machinga wanaouza vifaa, mavazi mpaka chakula kwa wananchi. Miongoni mwao wanauza bidhaa mpya na wengine mitumba.

Mtu halazimishwi kununua bidhaa ila ni kutokana na imani, mahitaji na nia yake, hivyo hujikuta amenunua kitu kwa kukiona kwa macho, na kuridhika. Na hiyo ni kwa bidhaa zisizo za chakula.

Ni wachache sana wanaoweza kubaini kuwa chakula fulani ni salama au si salama kwa kukiangalia kwa macho. Na ndiyo maana watu wengi hujikuta wamedhurika kwa kula chakula kisichofaa ama kilichoharibika au chenye sumu.

Imetokea baadhi ya wachuuzi wasio waaminifu kuuza chakula husUsan kitokanacho na wanyama wasioliwa. Mathalan, wako waliokamatwa wakiuza nyama ya mbwa na kuchukuliwa hatua.

Ziko taratibu za kiafya kwa mfano, ambapo Serikali imeweka utaratibu, kwamba katika kila machinjio ya wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo, wanakuwapo wataalamu wanaopima ubora, usalama na uhalali wa nyama.

Lakini bado pia wako wanaochinja kinyemela na kupenyeza nyama madukani. Yaweza kuwa ya mnyama mgonjwa au kibudu.

Ndugu zetu wa Kiislamu huamini kuwa mnyama aliyechinjwa na asiye wa dini hiyo, ni haram. Hiyo ni imani yao na inastahili kuheshimiwa. Hivyo kama ng'ombe, mbuzi au kondoo atakuwa amechinjwa na asiye Mwislamu, nyama yake ni haram kwa Mwislamu.

Hivi sasa limeibuka wimbi Dar es Salaam, la baadhi ya wachuuzi kupita mitaani wakihanikiza kuuza utumbo. Wanunuzi wananunua, kuupika na kuufakamia, bila hata kuthibitisha ni wa mnyama gani.

Lakini pia wanaufakamia bila kuthibitisha mnyama mwenye utumbo unaouzwa amekufa kwa kuchinjwa, kwa ajali au ugonjwa! Mchuuzi naye hana uhakika utumbo huo ni wa mnyama gani. Na kama anajua ni siri yake. Tujiulize hasa wale wapenzi wa nyama ya nguruwe, almaarufu kitimoto, ni wapi wameshuhudia utumbo wa mnyama huyo ukichemshwa, kukaangwa, kuchomwa au kupikwa? Kama hawajashuhudia je, utumbo huo hupelekwa wapi?

Yawezekana unaouzwa mitaani. Nani anajua? Kwa sababu hakuna anayeweza kuthibitisha mtaani kuwa mchuuzi anauza utumbo wa nini na hakuna anayeweza kuutofautisha wa mnyama huyu au yule.

Lakini pia samaki. Kuna wavuliwao salama na wengine kwa sumu na baruti. Nani athibitishaye?

Pengine hata viongozi mitaani nao huitisha utumbo na samaki na kununua bila kuhoji unatoka machinjio au duka au soko lipi la nyama na samaki.

Ni mpaka hapo itakapobainika kuwa watu wameshafakamia sana utumbo wa mbwa au samaki wenye sumu, ndipo viongozi watakaposimama kuzungumza.

Mara nyingi viongozi wetu litokeapo la kutokea, ndipo hujitokeza kusema: "Tulishnawaonya lakini hawasikii...leo narudia tena kuonya...sitaonya tena... hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika kuuza bidhaa hizi tena!"

Hizo huwa ni nadharia za viongozi wetu ambao hutafuta kiki katikati ya matatizo. Iko wapi amri ya kukataza wachuuzi wa silaha kama mapanga, sime na visu barabarani?

Mpaka leo silaha zinauzwa barabarani kama karanga, kama nyanya, zinauzwa mpaka kwenye baa, ambako baadhi ya watu huwa na akili tofauti.

Tuombe Mungu siku mchuuzi wa sime asipite baa akakuta fumanizi. Yatatoka matamko mengine ya kupiga marufuku. Tutakuwa tayari tumechelewa. Alamsiki!

# Serikali yagharamia mazishi anayedaiwa kupigwa na polisi

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MWILI wa kijana, Enos Misalaba, aliyefariki dunia kwa madai ya kupigwa na askari polisi Chato, mkoani Geita, umezikwa nyumbani kwao Nyabugera, huku serikali ikigharamia mazishi hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, ni miongoni mwa viongozi wa serikali walioshiriki mazishi hayo na kutoa salamu za pole kwa ndugu na jamaa.

Kijana huyo alifariki dunia Machi 28, mwaka huu, wakati akipatiwa matibabu kwenye Kituo cha Afya Muganza, ikiwa ni siku moja baada ya kukamatwa na kuwekwa kwenye mahabusu ya kituo kidogo cha polisi Muganza kutokana na tuhuma za kukutwa na mali inayodaiwa ya wizi.

Kifo cha kijana huyo kilisababisha taharuki kubwa kwa jamii, jambo lililosababisha baadhi ya wananchi kugoma kufanya mazishi yake na kushinikiza mwili huo kurejeshwa kituo cha polisi kwa madai kuwa ndiyo chanzo cha umauti wake.

Askari polisi waliuchukua mwili wa kijana huyo na kuupeleka chumba cha kuhifadhia maiti kwenye Hospitali ya Wilaya ya Chato.

Hata hivyo wananchi hao walivamia kituo hicho cha polisi kisha kuvunja na kuchoma nyaraka mbalimbali zikiwamo pikipiki zilizokamatwa kwa makosa mbalimbali.

Katika tukio hilo mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Haruna Mtondo, alifariki dunia baada ya kupigwa risasi, huku wengine watatu wakijeruhiwa kwa risasi wakati polisi wakijihami kutokana na vurugu hizo.

Wananchi waliojeruhiwa ni Elisha Lyara, Hussein Marco pamoja na Asteriko Fitina, ambao kwa sasa hali zao zinaendelea vizuri baada ya kupatiwa matibabu.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Shigella alifika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato kuwajulia hali majeruhi hao kisha kuagiza gharama zote za matibabu zigharamiwe na serikali.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Katemwa Kata ya Muganza, Shigela aliwaonya wananchi kutorudia kufanya uvamizi kama huo, huku akiwasihi iwapo wana malalamiko yoyote ni vyema wakafuata taratibu na sheria.

"Natambua tukio hili limetokana na baadhi yenu kutoamini ripoti ya chanzo cha kifo cha mpendwa wenu iliyotolewa na wataalamu wetu wa afya, hata hivyo hamkuomba kurudiwa uchunguzi wa chanzo cha kifo...

Lakini kwa kutambua hilo serikali imeamua kuleta madaktari bingwa wa upasuaji kutoka ngazi ya taifa ambao wanashirikiana na madakatari bingwa wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato kurudia uchunguzi ili kubaini kilichosababisha kifo" alisema Shigella.

Baada ya kufanya mazungumzo na wananchi hao, Shigella alishiriki mazishi ya kijana huyo, kisha kutoa Sh. milioni moja ikiwa ni ubani kwa msiba huo.




Wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga, wakiwa wamepanga bidhaa zao pembezoni mwa njia ya waenda kwa miguu karibu na kituo cha daladala cha Congo, Mtaa wa Msimbazi , Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taasisi yadhamini mikopo bil. 3.4/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS Trust) inayojihusisha na kuchochea uwekezaji na ukuaji katika sekta ya kilimo kupitia upatikanaji wa fedha imefanikisha kutoa dhamana za udhamini wa mikopo ya kilimo biashara 66,077 ambayo imewafikia wanufaika milioni 3.4.

Meneja Maendeleo ya Biashara wa PASS Trust, Herman Bashir, alisema hayo jana wakati akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Yohana Kaduma, kwenye uzinduzi wa kampeni ya Kijanisha Maisha kwa wadau wa sekta ya kilimo mkoani Singida na Programu ya Ukuaji wa Kijani Shirikishi Kanda ya Kati na Mashariki.

Alisema kati ya wanufaika hao, asilimia 51 ni wanawake na kwamba zimetengenezwa ajira milioni 2.7 nchi nzima na katika mkoa wa Singida wajasiliamari 6,620 wamefikiwa. Bashir alisema tangu kuanza kwa mradi huu wa ukuaji wa kijani shirikishi mwaka 2021 hadi Desemba, mwaka jana, tayari wanufaika 516,106 ambao kati yao asilimia 71 ni wanawake, wamenufaika na dhamana ya kijani (Green Technology Guarantee).

Pia alisema katika kipindi hicho PASS Trust imetoa mafunzo ya Ukuaji wa Kijani Shirikishi kwa zaidi ya maafisa 500 wa benki washirika Tanzania nzima.

lisema kuwa wakulima wananufaika na PASS Trust kwa kuwekewa dhamana ya mikopo ya kilimo, mifugo na uvuvi kupitia benki mbalimba nchini kwa kutoa dhamana ya hadi asilimia 80 ya mikopo kwa wakulima, wavuvi, wafugaji na wenye viwanda wanaozalisha kwa kufuata kanuni za uhifadhi wa mazingira.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema serikali ya mkoa inatambua na kuthamini mchango wa PASS Trust kupitia dhamana zinazotolewa kwa wajasiliamari wa kilimo ambazo zimekuwa daraja muhimu sana katika kuwaunganisha wakulima hasa ambao dhamana zao hazitoshi kuweza kubufaika na mikopo inayotolewa na benki.

"Nazipongeza taasisi za fedha kwa mchango zinapitia katika sekta hii ya kilimo kwa kuunga mkono maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kupunguza riba katika mikopo ya kilimo kwa hadi asilimia 9," alisema.

Serukamba aliwaomba wadau wa kilimo kuendelea kufanya shughuli za uzalishaji kwa kuzingatia kanuni za ukuaji wa kijani shirikishi kama ambayo PASS Trust inazingatia katika suala la utunzaji mazingira.

## DC apigia debe uwekezaji kilimo

**Na Steven William,** NACHINGWEA

SERIKALI wilayani Nachingwea mkoani Lindi imesema inawakaribisha kwa mikono miwili wawekezaji kuwekeza kwenye sekta za madini na kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, alitoa wito huo juzi katika ziara ya kijiji kwa kijiji yenye kaulimbiu "Ulipo Nipo Toa Kero Yako Sema Kweli".

Moyo alisema wilaya ya Nachingwea ina aina zote za madini ambayo yanatakiwa sokoni, hivyo anawakaribisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ya madini. Pia alisema wilaya ya Nachingwea ina utajiri wa ardhi unaoifanya kuwa moja ya wilaya tajiri baada ya miaka mitano.

Kadhalika, Moyo alisema Nachingwea imebarikiwa utajiri wa kila aina hivyo ni juhudi binafsi zinatakiwa ziongezwe kwa wananchi.

Alisema maono yake, katika muda atakaokuwa wilayani hapa, ni kuhakikisha wilaya hiyo inapata wawekezaji wengi kwenye kila sekta ili kuzitumia fursa za kiuchumi zilizopo kwa mujibu wa malengo ya serikali ya kuvutia wawekezaji.

Katika hatua nyingine, Moyo aliwataka wananchi wa Nachingwea kujituma kulima mazao mchanganyiko ili kuondokana na tatizo la njaa ambalo limewakumba mara kwa mara.

Alisema wilaya ya Nachingwea imebarikiwa kuwa na ardhi yenye rutuba ambayo haitumiwi vilivyo kuzalisha mazao ya chakula na biashara, hivyo kusababisha wananchi hao kila mara kuomba chakula cha msaada kwa serikali.

"Mimi sitaki kusikia wananchi wanalalamika kuhusu njaa wakati ardhi ina rutuba kuliko hata baadhi ya maeneo mengine ambako huwezi kusikia wanaomba msaada wa chakula. Sasa tutabanana hadi tunaondokana na njaa," alisema.

# MAISHA

APRILI 2, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14


## Futari viazi mviringo

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



## Safisha dirisha ung'arishe nyumba




## KATUNIKA

Ukurasa 16



# NYWELE ZINAZONAWIRI

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | 3 | 1 | 4 |
| 4 | 1 | 2 | 3 |
| 1 | 4 | 3 | 2 |
| 3 | 2 | 4 | 1 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | W | A | ■ | F | A | A |
| A | ■ | ■ | ■ | U | ■ | N |
| W | ■ | M | A | M | ■ | Z |
| I | B | A | ■ | B | E | I |
| N | ■ | M | T | O | ■ | S |
| G | ■ | B | ■ | ■ | ■ | H |
| U | Z | A | ■ | J | A | A |


## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ■ | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | ■ | | | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ANA, MBA, MKE, CHA, MEI, PAO, MTI, TUA, MSOMI, PAMBA, CHUTAMA, ASHIKWE

## TOA TOFAUTI 5





## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 1 | |
| | | 4 | |
| 4 | | | |
| 2 | | | |

## WATOTO

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

## CHEKA

JOHN alikwenda sokoni kununua nyanya na mambo yalikuwa hivi.

John: Nyanya zinauzwa kiasi gani?

Muuzaji: Kilo shilingi 1500

Kijana: Nimegizwa unisagie tunataka kwenda kula na chipsi nyumbani

Muuzaji: Kijana usitanie kazi za watu

Swali
Chaza inapatikana sehemu gani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Kuna tabia unapaswa kuziacha ili ufanikiwe

KARIBU tena msomaji wangu

Mungu anasema katika moja ya neno lake: "Siri ya BWANA iko kwao wamchao." Tukiwa tumeuanza mwezi Aprili, 2023 ziko siri ambazo unapaswa kuzijua. Kubwa zaidi, lazima utambue kuwa kuna maandalizi unayopaswa kuyafanya kukusaidia kule unakotaka kwenda.

Hakuna mwanadamu anayependa kuwa mtalii wa mwaka na mwaka ni namba.

Mtumishi mmoja wa Mungu akasema, 'hakuna mwaka mpya ila kuna mtu mpya'. Maana yake ni nini? Usipoangalia unaweza kujikuta ukiwa vile vile, mambo ni yale yale, maisha ni yale yale hakuna kilichobadilika kwenye maisha yako.

Kushinda au kushindwa kunategemeana na maandalizi uliyo nayo. Ndio maana watu wanapofunga ndoa, kabla ya kufikia kwenye ndoa, wanapitishwa kwanza kwenye darasa la ndoa.Yapo mafundisho fulani usipoyapata huwezi shinda kwani lazima upate maelekezo kwanza.

Sasa ni siri gani za maandalizi unapaswa kuzijua unapoingia mwezi huu wa nne 2023. Siri namba moja; kubadili mavazi. Huwezi kuwa na divai mpya ukaiweka kwenye kiriba kikuu kuu. Hapo lazima utafeli. Divai mpya inaendana na kiriba kipya.

Neno la Mungu katika Mathayo 9:17 linasema: " Wala watu hawatii divai mpya katika viriba vikuukuu; na kama wakitia, vile viriba hupasuka, divai ikamwagika, na viriba vikaharibika; bali hutia divai mpya katika viriba vipya, vikahifadhika vyote."

Yako mavazi unapaswa kuyavaa ili uwe mtu mpya na mwaka mpya huu uendane na wewe. Mwaka huu mpya hakuna mwanadamu mwenye akili timamu anayependa abakie pale pale. Mwaka unapovuka kuingia mpya watu hushangilia wakitamani kuwa wapya.

Mwaka mpya hushangiliwa na watu wote, wengine wacha Mungu, wengine wenye dhambi, kila mmoja kivyake. Watakatifu wako nyumba za Mungu za ibada na wengine wako beach wakisherehekea mwaka mpya. Hii ni kwa sababu kila mmoja anatamani mwaka huu mpya apige hatua mpya.

> **Hakuna mwanadamu anayependa kuwa mtalii wa mwaka. Na mwaka ni namba.**

Viko vitu katika maisha yako, usipokubali kuviacha hautabadilika, hautauona upya. Kuna mambo fulani, mazoea fulani, kuna tabia fulani upo nazo na usipoziacha utabaki wewe yule yule. Huwezi kutarajia mambo mapya kwa tabia za zamani, haiwezekani!

Kama hutakubali kuachia baadhi ya vitu, kama hutakubali kubadilisha baadhi ya mitizamo yako, Kama hutakubali kuondoa baadshi ya vitu vinavyokuzuia, hautabadilika, hautauona mwaka huu mpya kuwa wa faida kwako. Utakuwa ni yule yule kwa sababu wewe ni yule yule.

Mwombe sana Mungu mwaka huu akupe mambo mapya. Huwezi kutarajia mambo mapya kwa tabia za zamani. Kama yapo mambo mapya, basi kuna vitu katika maisha yako ukubali kuvidondosha, kuviacha.

Kuna baadhi ya tabia ukubali kuziacha, kama ni uvivu, ulevi, uzinzi, uwongo, usengenyaji, wizi, ulaghai na kadhalika. Ukichukua hatua hiyo, utaona mambo yanakuwa mapya!Utaona baraka mpya, utaiona imani mpya. Lakini ukikaa na kubakia hivyo hivyo, maana yake wewe ni yule yule utataka vitu vile vile.

Haiwezekani hata siku moja kutumia mbinu zile vile, tabia zile zile, bidii ile ile, nguvu zile zile upate matokeo mapya! Ili upate matokeo mapya lazima upate vitu vipya viingie ndani yako! Usimwambie Mungu badilisha maisha yangu, mwambie Mungu akubadilishe ili ujibadilishe kimaisha.

Mungu akikubadilisha, mambo yako yatabadilika yenyewe sawia. Maana zipo tabia zinavuta pesa, utajiri, watu wema. Hata kama hutawaomba kila mtu atakufuata kwa sababu palipo mzoga ndipo tai wanakuja wengi. Yaani unaomba Mungu, niletee watu wazuri, lakini tabia zako ni za zamani, tabia zako zinafukuza watu.

Ukipewa pesa unatapanya, Mungu atakupa nini na utabaki na nini? Unamwambia mtumishi wa Mungu niombee nipate pesa, tatizo siyo upatikanaji wa pesa, bali tatizo ni wewe. Ukibadilika pesa zinakaa, wateja watarudi kwako.

***Bila shaka umejifunza jambo hapo. Hadi wiki ijayo. Heri ya Mwaka Mpya 2023. Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Tuendelee kutafuna, kutafuta au tuwajibishane kwanza?

AAAH wachukue hatua tu, hii sasa inatosha! Ni maneno yanayotawala vinywa vya Watanzania wengi hivi sasa. Lakini inaweza kuwa dhana ya ajabu iwapo kuna mambo yatatekelezwa kwa sababu wanazozijua wengine na kwa mtindo wanaoujua wao.

Tatizo letu linaweza kuwa lile lile la kusukumwa na utashi wa kisiasa wa kusema na kukosoana hadharani au mitandaoni na kisha kuliacha bila kuchukua hatua stahiki za kuwajibishana.

Tusilifanye jambo linalotuhusu sisi Watanzania kuwa gumu. Tuanze kudhibiti hali hii kwa kuziba mianya na kuwajibishana kwanza kwa sababu kila mmoja wetu aliyeisikia hata kwa juu juu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iliyokabidhiwa na Charles Kichere kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Jijini Dar es Salaam, Machi 29, mwaka huu, anaumia moyo wake.

Wengi wanajiuliza, wanasononeka moyoni huku wanatembea wakijihoji kama wagonjwa wa akili, hivi hao wahusika wanaotajwa kwenye hayo madudu kila mwaka huwa wanaishia wapi baada ya ripoti ya CAG kutolewa? Si wanajulikana, wanafichiana siri au wanaogopana?

Kwa mtu wa kawaida, ripoti hii ya CAG inaweza kuwa na maana kubwa. Inaweza kuwa na matumaini makubwa na inaweza kutupa picha halisi ya nini kifanyike kudhibiti upigaji wa pesa za umma, hasara yanayopata mashirika ya umma na uzembe unaofanywa na watendaji wachache wa umma katika serikali za mitaa.

Yako madudu ya kutisha katika sekta na taasisi mbalimbali za umma zikiwamo za maji, Bwawa la Mwalimu Nyerere na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Madudu ambayo yamekuwa yakijirudia kila mwaka kwenye ripoti za ukaguzi na kuonekana kuwa jambo la kawaida.

Mathalani, katika mradi mkubwa wa usambazaji maji katika wilaya za Mwanga, Same na Korogwe wenye thamani ya Sh. bilioni 263.5 zinazofadhiliwa na serikali ya Tanzania na wadau wa maendeleo kama Benki ya Kiarabu inayosimamia maendeleo ya nchi za Afrika (BADEA), Mfuko wa OFD unaojumuisha nchi zinazozalisha mafuta (OPEC) na Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa SAUD na Mfuko wa Misaada wa Kuwait. Mradi huo tangu uanze kutekelezwa Desemba 17, 2014 na kutakiwa kukamilika Machi 4, 2021 hadi sasa haujakamilika.

Haiyumkini, kuna mashirika 14 ya kibiashara mwaka 2020 hadi mwaka 2022 likiwamo TRC, ambalo mwaka 2020/21 lilipata hasara ya Sh. bilioni 22.782, huku mwaka 2021/22 likipata hasara ya Sh. bilioni 31.295 hali iliyoathiri mitaji iliyowekwa na serikali.

Haitoshi, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), liliongeza muda wa mkandarasi katika Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere hadi Juni 18, 2023 kutokana na makadirio yasiyo halisi na kasi ndogo ya utekelezaji.

Ukweli ni kwamba wajanja wachache wameamua kujitajirisha kwa njia haramu na ni kipofu peke yake ndiye anayeweza kusema haoni. Kwa mfano, ripoti ya CAG inaeleza kwamba ukaguzi wake umebaini kuwa Sh. bilioni 11.07 hazikuwekwa katika akaunti za benki na wakusanyaji wa mapato kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa 98. Hiyo inatokana na ufuatiliaji duni wa kutofanyika kwa uwasilishaji wa hesabu wa mara kwa mara.

Kwa jicho la tatu, naona bado yako mambo yanajirudiarudia na hayatoi taswira nzuri kwa nchi yetu kwa sasa na huko tuendako. Jambo moja kubwa ni kwamba, tunawatwisha mzigo viongozi wetu, tunasahau kwamba na wao ni Watanzania waliolelewa katika misingi ya haki na usawa, umoja na mshikamano.

Uwezo wa kufikiri ni mojawapo ya tunu kubwa ambayo binadamu amepewa kupitia maumbile yake. Ubongo unao uwezo mkubwa wa kuifanya kila sehemu ya mwili wa mwanadamu kuitenda kazi yake vyema na wakati huo huo kuwa mtambo mahususi wa kuchuja mambo, kutafsiri matukio, kuhifadhi habari na kuandaa mipango kinadharia na kivitendo. Katika haliyo, nimejikuta nikijiuliza eti, tuendelee kutafuna, kutafuta au tuwajibishane kwanza?

Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.

**Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com**


**Simu ya mkononi: +255 767 535490**



Magauni ya harusi ya rangi ya njano huleta mvuto wa kipekee kwa bibi harusi. Pichani ni baadhi ya magauni yanayovutia kuvaliwa siku ya harusi.

# MITINDO





## Ukiperuzi tu, unapendeza

SANAA ya mitindo ya mavazi ni miongoni mwa vitu vinavyosaidia vijana kujipatia ajira na kujiingizia kipato.

Vijana wengi wamehamasika na kujichanganya katika tasnia hiyo, na hivyo kuondoa dhana kwamba tasnia ya mavazi hailipi.

Wakitumia teknojia ya kisasa ya mawasialiano, watu wanakutanishwa katika majukwaa ya mitandao ya kijamii kujadili, kubuni na kufanya biashara ya mavazi.

Kimsingi mambo yamekuwa moto, kila aina ya mavazi unaweza kuona katika kiganja chako, unachotakiwa wewe ni kuuliza bei na kutoa oda, na saa chache unajikuta unapata nguo mpya.

Kutokana na mabadiliko hayo, zipo changamoto ambazo zinaonekana kuwa kikwazo kwa vijana katika kujikomboa kiuchumi kupitia mitindo katika mitandao.

Mbunifu wa mavazi, Irada Mahadhi, anasema kwa kutumia teknolojia ya kisasa mtu anaweza kubuni, kutangaza na kuuza kwa muda mfupi zaidi, tofauti na zamani.

Anasema kikwazo kikubwa katika soko la mtandaoni baadhi ya watu wanakuwa sio waaminifu kwa kuuza mavazi tofauti na mteja alivyoagiza au nguo kukosa ubora unaokubalika.


Hata hivyo anathibitisha kwamba soko la mitandaoni limekuwa kubwa na linasababisha hata wabunifu kupata wakati mgumu wa kutengeneza nguo zinazoendana na wakati uliopo.

URMEBO

Na Mary Geofrey

# NYWELE ZINAZONAWIRI

## mbegu za papai hutibu mba



UCHAFU unaoganda kwenye nywele unaojulikana kama mba, ni miongoni mwa mambo yanayosababisha ngozi kukosa muonekano mzuri.

Mba humfanya mtu kujikuta akijikuna kila wakati kutokana na kuwasha.

Kitaalamu mba ni aina mojawapo ya magonjwa yanayoambukizwa na fangasi ambao husababisha muwasho.

Wanawake wengi wanakumbana na matatizo haya ya mba, kutokana na kupaka aina ya vipodozi vinavyowaletea athari katika ngozi zao.

Unapokumbana na tatizo la namna hii ni vizuri kujipaka dawa zinazofaa badala ya kutafuta krimu ambazo ni hatari zaidi.

Mbegu za papai ni tiba nzuri na ya asili ambayo haiwezi kukuletea madhara zaidi.

**Jinsi ya kuondoa mba kwenye ngozi ya uso**

Mbegu za papai ni dawa ya asili inayoweza kutibu ngozi yako na kukuondolea tatizo la kuwashwa au mabaka yanayokukabili.

Namna ya Kutumia Mbegu za Papai

Unachotakiwa kufanya ni kuchukua mbegu za papai na kuziponda kwa kutumia kinu au brenda.

Kisha anza kujipaka sehemu ambako kuna mabakabaka ya mba huo.

Unaweza kurudia kila mara hasa wakati wa kulala hadi utakapoona mbao huo unaondoka na kuwa na ngozi nyororo badala ya kutumia vipodozi vikali.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Futari viazi mviringo

WIKI iliyopita tulielekezana namna ya kupika futari ya ndizi ambayo haichukui zaidi ya dakika 25 kuiva na kuanza kuliwa.

Leo katika safu hii, tunaelekezana aina nyingine ya futari ya viazi mbatata ambayo nayo haihitaji muda mrefu kuandaa hadi kuanza kula.

**Viazi mbatata**

Mahitaji ni viazi mbatata kulingana na ukubwa wa familia ya watakaokula, nyanya, vitunguu, pilipili hoho, karoti, mafuta ya kupikia, maji safi, chumvi, nazi na pilipili mtama.

**Maandalizi**

Menya viazi, unaweza kuvikata au kuviacha vizima kulingana na unavyopenda.

Vioshe vizuri kwa maji safi na tayarisha nyanya, vitunguu, hoho na karoti

Bandika sufuria ya kupikia jikoni, weka mafuta yakichemka weka vitunguu maji, vikiiva kiasi weka vitunguu saumu, kisha acha viive hadi viwe na rangi ya hudhurungi (brown).

Weka viazi mbatata kwenye mchanganyiko wa vitunguu koroga kwa muda na uviache kwa muda wa dakika 10 hadi 15 hadi vikaukie mafuta kisha weka nyanya hakikisha unaweka moto uwe wa kutosha ili ziive.

Funika kwa dakika tano, geuza kisha weka hoho, karoti na tui la nazi kwa pamoja kisha funika, hadi liive geuza na hakikisha vimechanganyika na vimebaki na mchuzi mzito kisha viipue tayari kwa kuliwa.

Futari hii unaweza kunywa na chai, uji, maziwa au supu na ukafurahi kufuturu kwako.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Safisha dirisha ung'arishe nyumba

DIRISHA ni moja ya vitu vinavyochangia kung'arisha nyumba. Ili dirisha liendelee kuwa bora na kung`arisha nyumba lazima lisafishwe.

Endapo usipoweka kipaumbele katika jambo hilo usishangae kuona mvuto wa nyumba yako kuanza kufifia kidogokidogo na mwisho wake ukaichukia nyumba kabisa.

Usafishaji wa dirisha ni lazima uwe na muda maalum ambao hakuna jua kali kwa sababu unaposafisha wakati wa jua kali, maji unayominia katika dirisha lako hukaushwa hata kabla ya kupitisha sponji na hivyo itakuchukulia muda mwingi na pia haliwezi kung`aa vizuri na huacha ukungu.

Wakati unasafisha unatakiwa uwe pia na dawa maalum au kama unatumia maji si vibaya ukadondoshea kidogo vitone hata viwili vya maji maalum yenye mchanganyiko wa limao, maarufu kama 'vinegar'.

Baada ya hapo unalowanisha 'sponji' yako ama kitambaa laini kwa kuchovya kwenye maji hayo na kuanza kusafisha katika dirisha lako.

Hakikisha unasafisha kuanzia juu kushuka chini, ili uchafu wote utiririkie huko kwa sababu kufanya hivyo kutakuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakaodondokea kwenye sehemu ambayo umeshasafisha tayari.

Kama eneo la dirisha unalotaka kusafisha ni chafu sana ama kuna vumbi jingi au utando wa buibui, futa kwanza kwa kitambaa kikavu kabla ya kusafisha na maji.

Uwe makini kuchunguza uchafu ulioko kwenye kona za madirisha yako.

Epuka sana kuweka maji mengi kwenye sponji ama kitambaa chako unachotumia kusafishia ili yasimiminikie chini sehemu ambayo siyo ya dirisha iwe ukutani ama sehemu nyingine isiyohusika.

Hakikisha unasuuza na kukausha dirisha lako kwa kutumia kitambaa kikavu na laini na baada ya hapo rudia tena kwa ajili ya kuling'arisha.

Kama utakuwa na dawa maalum ya kusafishia itapendeza zaidi kuipulizia kidogo katika dirisha lako huku ukifuta kwa kutumia kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzi.

Hakikisha dawa unayotumia kusafishia ni ile ambayo haiwezi kuharibu ama kupausha mbao za dirisha lako.

Kama dirisha lako ni la kioo, hakikisha sponji ama kitambaa ulichotumia kusafishia kioo ni tofauti na kile unachosafishia kwenye fremu ama kona za dirisha lako.

Katika maeneo ya fremu na kona, safisha kwa kutumia kitambaa kigumu zaidi ambacho kitabeba uchafu wote kwa sababu eneo hilo huhifadhi uchafu mwingi.



## Yajue maua yanayopandwa majini

**Na Restuta James**

KWA wapenda maua neno 'hydroponics' haliwezi kuwa geni kwao kwa kuwa ni lugha ya kitaalamu kwa mimea inayokua ndani ya maji pasipo kuweka udongo.

Upandaji huu wa maua ni mzuri hasa kwa 'walevi' wa mimea kwani ni rahisi kuiweka popote ikiwamo jikoni, chumbani au chooni (kwa maua yanayosafisha hewa).

Upandaji huu wa mimea au maua haya una ladha ya pekee ndani ya nyumba kutokana na kwamba yanatumia zaidi majagi ya udongo.

Wataalam wa bustani wanaeleza kuwa upandaji huu unavutia na kuongeza 'usafi' ndani ya nyumba kwa kuwa ua na chombo vyote ni lazima viwe visafi wakati wote.

Wanaeleza kuwa ubunifu unaweza kumsaidia mlevi wa maua kiasi cha kuanzisha bustani ya rosemary jikoni.

Hii ni kwa sababu mbali ya kujipatia kiungo 'fresh' jikoni kwako kama utaamua kujiongeza kidogo.

Wanashauri kwamba sehemu nzuri ya kuweka maua haya ni kona yoyote ya nyumba, kwenye 'console', meza ya chakula na meza ya vipodozi.


Kwa watu wa saluni, upandaji huu unaongeza thamani na kuwavutia wateja kwani maua au rangi ya ukijani inatajwa kutuliza sana akili.

DONDOO MUHIMU

- Ni lazima ukumbuke kubadilisha maji kila wiki au walau kila baada ya wiki mbili. Katika hili, hakikisha unatenga siku yako ya mapumziko kuwa ndiyo ya kubadilisha pia maji ya maua.
- Hakikisha ua au mmea wako unauweka karibu na dirisha ili uweze kupata jua na kupata afya nzuri.
- Maua haya yanawekwa kwenye orodha ya usafi na umaridadi usio kifani.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
'UNGEYAVIMBIA MAFURIKO KAMA ULIVYOZIMBIA NOTISI ZA MWENYE NYUMBA WAKO!'
WE'CHONGA TU. NAHAMIA N'TWARA NIONE KAMA UTASAVAIVU!
HUYU SI NTU!
NIME'NSIKIA!
BABA KWENYE UPIGAJI HUYU HANA AIBU ANAONGEZA SIFURI MPAKA ANASTUKIWA! HAKOMI WALA HANA UOGA... BABA MUONDOLEE PEPO LA UPIGAJI AWE NA HOFU NA MALI YA UMAA...
KWA MUDA TU BABA
NYIE MNAACHA KUCHANGANUA BEI ZA UNGA, MCHELE NA MAHARAGWE ILI TUISHI KAMA ZAMANI MNABISHANA MPIRA TU!
HILI SIO BUNGE LA BAJETI KAKA
TATIZO KILA MTU HUMU MJUAJI, WE UNADHANI USIPOSEMA UTASIKIKA?
WEWE ULIYE-SIKIKA MBONA MANDONDO BEI HAIJAPORO-MOKA?
HATUTAKI STRESS HATA TUKIONGEA BEI HAITASHUKA ACHA TUPIGE SOGA TUJILIWAZE
UJILIWAZE? HAPO ULIPO TUMBONI PATUPU UTAANGUKA UTUFIE HUMU!
MBAGALA
JAMANI MAKELELE WATU TUMEFUNGA NSIJE NKAMNASA MTU MAKOFI...
UNATAKA NDUNDI?!
KWA IMANI YAKO SIRUHUSIWI KUKUUZIA MSOSI MUDA HUU MPAKA JIONI.
TOKA UZALIWE HUJAWAHI KUSIKIA NENO "KOBE" KIPINDI KAMA HIKI HUWA 'LINATRENDI SANA!'
KWA STAILI HII ACHA WATU SIKU HIZI WAFUTURIE NDANI HA HA HAAAA!
AMMA!!! KWA TAARIFA YAKO MWALIKO WA MSELA 'KADI UKAUZU WAKE'
NASKIA ULIKUWA UNATAKA KUJIUA ULIPOSIKIA NIMEPEWA LIFTI NA MTALAKA WANGU!
HUYO ALOKWAMBIA KAMA NI MWANA'NKE ANANTAKA! UNAVYOLIONA HILI POZI LA KUFA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...TUNDU LA RIZIKI HALIZIBWI KWA FITINA...

## Idadi waliokufa Malawi yaongezeka

**LILONGWE,** MALAWI.

IMEELEZWA watu 700 wameripotiwa kupoteza maisha tangu Kimbunga Freddy kuipiga Malawi mwezi ulipita.

Hata hivyo, Umoja wa Mataifa ulisema huenda watu 1,200 wamefariki dunia katika taifa hilo la kusini mashariki mwa Afrika kutokana na mkasa huo.

Taarifa ya serikali inaonyesha watu 676 wamekufa na wengine 538 bado hawajulikani waliko tangu Kimbunga Freddy kuikumba Malawi.

Kimbunga hicho kimesababisha mvua kubwa kusini mwa nchi hiyo ambayo imenyesha kwa siku sita. Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kiutu ya Umoja wa Mataifa inatarajia idadi ya vifo kuongezeka hadi kufikia watu 1,200.

Zaidi ya watu nusu milioni wamelazimika kuyaacha makazi yao nchini humo. Shirika la Save the Children linakadiria kwamba watoto 500,000 kwa sasa hawawezi kwenda shule.

Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa Ulimwenguni lilitabiri kwamba kimbunga Freddy, kitakuwa cha muda mrefu tangu kuanza kwa rekodi za hali ya hewa.

Kimbunga hicho kimepiga eneo la kusini mashariki mwa Afrika kwa mara mbili katika mwezi wa Machi.

Tufani hiyo yenye nguvu imesababisha uharibifu mkubwa nchini Malawi na Msumbiji.

**DW**

## Sakata la Trump kufunguliwa mashtaka laibua sura mpya

**WASHINGTON,** MAREKANI

WANASHERIA wa rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, wamesema kiongozi huyo yuko tayari kupambana.

Walisema kutokana na kinachoendelea mteja wao hatokubali kufanyika kwa makubaliano nje ya mahakama.

Kauli hiyo ilitolewa na wanasheria hao, muda mchache baada ya mahakama kuamua kuwa Trump (76), ana kesi ya kujibu.

Trump ambaye anakusudia kuwania tena urais kwenye uchaguzi mkuu wa 2024, aliwashambulia waendesha mashitaka walioyaibua mashitaka hayo kuwa wana nia ya kuingilia uchaguzi huo.

Akitumia mtandao wake wa kijamii, Truth Social, Trump aliandika kwa herufi kubwa, "UINGILIAJI WA UCHAGUZI, MAHAKAMA YA KANGAROO!"

Aliongeza pia Jaji Manuel Marchal atakayesikiliza kesi hiyo anamchukia.

Jioni ya siku ya Aprili 4, Trump atatazamiwa kufunguliwa rasmi mashitaka, kuchukuliwa alama za vidole na kupigwa picha kwa ajili ya bango la mashitaka kwenye mahakama ya Manhattan.

Baada ya hatua hizo kutekelezwa, Trump atapandishwa kizimbani akiwa rais wa kwanza wa Marekani kukabiliana na mashitaka ya uhalifu.

Rais Trump anatazamiwa kutiwa pingu, tukio ambalo Wamarekani wengi wanalisubiri kushuhudia.

Joe Tacopina, mmoja wa mawakili wa Trump, alisema haamini kwamba waendesha mashitaka wataruhusu suala kama hilo kutokea.

Tacopina alisema kesi ya fedha za fidia iliyoletwa na Mwendesha Mashitaka wa Wilaya ya Manhattan, Alvin Bragg, dhidi ya Trump ina mapungufu mengi kisheria na rais huyo wa zamani angelikana kutenda uhalifu wowote. Uwezekano wa Trump kuwekwa kizuizini kunaongeza mashaka kwenye kampeni yake ya kuwania kurejea kwenye Ikulu ya White House.

Hasimu wake, Rais Joe Biden, alikwepa kuzungumza chochote kuhusiana na kesi hiyo.

Jopo la majaji jijini New York lilimuona Trump ana kesi ya kujibu siku ya Alhamisi kutokana na kumlipa fedha taslimu dola 130,000 mchezaji wa filamu za ngono ili kumnyamazisha wakati wa kampeni zake za urais mwaka 2016.

**DW**

# Russia yaongoza baraza la usalama

**NEWYORK,** MAREKANI

JARIBIO la Ukraine kuizuia Russia, kuchukua kiti cha urais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limeshindikana, baada ya taifa hilo lenye nguvu kukalia nafasi hiyo.

Katika utaratibu katika baraza hilo la wajumbe 15, huchukua nafasi ya urais kwa mwezi mmoja kwa kupokezana.

Mara ya mwisho Russia ilishika nafasi hiyo Februari 2022, na ndio ilianzisha uvamizi kamili ndani ya Ukraine.

Kutokana na hatua hiyo, Baraza la Usalama linaongozwa na nchi ambayo rais wake yuko chini ya hati ya kimataifa ya kukamatwa kwa madai ya uhalifu wa kivita.

Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu ambayo si taasisi ya Umoja wa Mataifa, ilitoa hati ya Vladimir Putin mwezi uliopita.

Licha ya malalamiko ya Ukraine, Marekani ilisema haiwezi kuizuia Russia kuwa mwanachama wa kudumu wa baraza na kutwaa kiti cha urais.

Wajumbe wengine wa kudumu wa baraza hilo ni Uingereza, Marekani, Ufaransa na China.

Jukumu hilo mara nyingi ni la kiutaratibu, lakini balozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa, Vasily Nebenzia, aliliambia shirika la habari la Tass kwamba alipanga kusimamia mijadala kadhaa, ukiwemo wa udhibiti wa silaha.

Alisema atajadili utaratibu mpya wa ulimwengu ambao, unakuja.

Wakati huo huo, Ukraine imeadhimisha ukombozi wa mji wa Bucha kwa wito wa kuwepo kwa haki baada ya uvamizi wa Russia uliosababisha vifo vya mamia ya raia na kuufanya mji huo kuwa kitovu cha ukatili wa vita.

Wakati wa hafla ya maadhimisho hayo mjini Bucha, Rais Volodymyr Zelensky, alisema kuwa hawataruhusu kusahaulika kwa matukio hayo na kuahidi kuwaadhibu waliofanya maasi hayo.

Aliongeza kuwa katika barabara za Bucha, dunia imeshuhudia uovu wa Russia.

Rais wa Moldova, mawaziri wakuu wa Croatia na Slovakia pia walihudhuria maadhimisho hayo.

Jina la Bucha linaibua ukatili wa jeshi la Russia tangu uvamizi kamili nchini Ukraine Februari 24, 2022.

Vikosi vya Ukraine vilivyoukomboa mji huo, vilikuta miili ya wanaume, wanawake na watoto katika barabara, majumbani na makaburi ya halaiki.

**BBC**



Papa Francis akitabasamu wakati akiwa ndani ya gari akirudi katika makazi yake baada ya kulazwa hospitali kwa siku tatu akipatiwa matibabu ya changamoto ya upumuaji. **PICHA: Vatican Media**

# Papa Francis aruhusiwa hospitali

**ROMA,** VATCAN

KIONGOZI wa kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amesema kwamba bado yuko hai baada ya kulazwa hospitalini kwa kusumbuliwa na matatizo ya upumuaji.

Kauli yake hiyo ya utani aliitoa wakati akitoka katika hospitali hiyo iliyopo mjini Roma baada ya kulazwa kwa muda wa siku tatu.

Alilazwa katika Hospitali ya Gemelli akiwa na matatizo ya kupumua.

Vatican ilitoa taarifa kuwa angetoka jana kulingana na matokeo ya vipimo.

"Sikuwa na hofu, bado niko hai," papa huyo mwenye umri wa miaka 86 aliwaambia waandishi wa habari na waombezi wa heri nje ya hospitali kabla ya kuruhusiwa kuondoka hospitali.

Alionekana akitabasamu na kupunga mkono kutoka kwenye gari, kabla ya kutoka nje kuzungumza na umati wa watu na kisha alielekea Vatican.

**DW**

MAKALA

# TUWE WAZALENDO KWA VITENDO



Na Magabilo Masambu

NENO uzalendo siku za hivi karibuni, limekuwa likitajwatajwa na kila aina ya watu, wengi wao wakiwa wanasiasa lakini inavyoonekana waliokuwa wazalendo kwelikweli, hawakuwa wakipiga mbiu za tuwe wazalendo badala yake uzalendo wao ulionekana katika matendo na maisha yao.

Kuwa mzalendo si kuvaa bendera wala nguo zenye rangi ya bendera ya nchi badala yake matendo na maisha yetu ya kila siku yaonyeshe kwamba sisi ni wazalendo. Kuvaa mavazi yanayoonesha rangi za nchi pekee bila matendo mema kwa nchi, hilo pekee linakuwa kichaka cha kuwadanganya watu ili kutenda mambo mabaya zaidi kwa nchi.

Nayasema haya kwa sababu ni hivi juzi tu tumesikia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ambavyo tumekuwa tukisikia miaka yote ikisomwa na baadhi ya mashirika ya umma yakituhumiwa katika ufisadi wa kutisha lakini mbaya zaidi, ama hatua zimekuwa hazichukuliwi au zinazochukuliwa pia zimekuwa haziridhishi kiasi cha kukomesha vitendo vya wizi wa mali za wananchi.

Lakini ukifuatilia, utabaini kwamba miongoni mwa wale wanaotuhumiwa wamo ambao wamekuwa wakiimbia nyimbo za uzalendo. Wamekuwa wakitumia mapambio hayo kutupumbaza ili waendelee kutafuna mali za umma, wakiibuka wanaimba nyimbo za uzalendo na mavazi wanavaa yenye rangi za bendera ya nchi. Haya masuala sasa yamekuwa ya kawaida, CAG anatwambia sisi wananchi kwamba pale wameiba hiki na kile, lakini hakuna hatua za waziwazi zinazochukuliwa. Nchi inakopa fedha kwa ajili ya maendeleo yake lakini wachache wanaojiona wao ni wajanja wanapiga pesa, kisha mikopo inaendelea. Kuna wakati baadhi wanasema hiyo mikopo hakuna mtu atalipa badala yake nchi ndiyo italipa. Unajiuliza nchi inalipa kutoka wapi? Watakaolipa si ni wananchi kupitia kodi? Kwa nini hatuwaonei huruma wananchi hawa maskini?

Jambo mojawapo linalorudisha maendeleo ya nchi nyuma ni pamoja na wizi wa fedha hizo ambazo ndizo zingejenga hospitali, barabara, maji safi na shule. Mambo mengine yote yanayohusu maisha ya Watanzania wote, lakini kila mwaka taarifa haijawahi kuacha kutaja upotevu wa pesa ama kuingia hasara kwa baadhi ya mashirika ya umma, sasa ni lini tutayafikia maendeleo ya kweli?

Kwa hiyo ndugu zangu watanzania na viongozi wa nchi hii, tujionee huruma sisi wenyewe hata kabla hatujaanza kuzungumza kuhusu mifumo ya kisheria. Kila mmoja aone anayo nafasi ya kujenga nchi hii kwa ajili ya kesho ya watoto na vizazi vyetu, leo unaweza kujiona unayo nafasi. Huwezi kujua kesho kama hautakuwapo ndugu zako wataishije, watapataje huduma nzuri za umma, watasomaje, watatibiwa wapi leo wanaweza kutibiwa kokote kwa sababu unazo fedha za wizi, lakini kesho hautakuwepo na hapatakuwa na mtu wa kuiba ili watibiwe kokote, tujenge maendeleo ya jumla yatakayo mfaa kila mmoja wetu, tusidhani kwamba sisi hayatatuhusu tunaona hivyo kwa sababu leo tunazo nafasi.

Kibaya zaidi, wezi wa mtaani wamejaa magereza, wengine wanauawa kwa kuchomwa moto tena wakati mwingine kwa kuiba kuku au wanafungwa kwa sababu wametukanana. Wale wanaotajwa kwenye taarifa ya CAG wanakula maisha mtaani na wanaambiwa waondoke tu wenyewe ikiwa na maana kwamba waamue ama wabakie au waendelee au wahamishwe kwa nini wasishitakiwe kama wezi wengine?

Nadhani katika makosa ya wizi mkubwa wa fedha za umma, sheria zibadilishwe pasiwapo na mambo ya faini, kwa sababu haiwezekani mtu kaiba Sh. bilioni nne akashitakiwa mahakamani akahukumiwa kulipa faini Sh. milioni nne au 10 kisha anaachiwa anaendelea kula kiasi kilichobaki. Hii ni dhihaka kwa nchi ni dharau kwa mahakama na majaji wote watakaokuwa wamehukumu kesi hiyo, lakini pia inachangia sana rushwa. Sasa itafika mahali hakimu anayekabidhiwa kesi ya Sh. bilioni nne anafanya sherehe kwake kabla ya kesi yenyewe maana anajua hii ni neema.

Vinginevyo nishauri, kama hatua zinakuwa hazichukuliwi ni bora CAG asiwe anasoma taarifa yake hadharani, badala yake awe anawasilisha kimyakimya kwa Rais maana sasa inakuwa na maana gani kama inasomwa kila mwaka na hatuoni hatua zikichukuliwa. Pili, huu utaratibu wa kuimba tuwe wazalendo wakati tunaona matendo hayasadifu ukweli huo tunaweza kuachana nao, kwa sababu mtu hawezi kuwa mzalendo huku akiona wapo watu wanaoibia nchi na hatua hazichukuliwi waziwazi.

Uzalendo unajengwa kwa namna mbalimbali. Moja ni usawa, usawa katika ujira na haki. Ujira wa kazi usipishane sana, lakini kwenye haki sheria zisichague kwamba kaiba huyu hatakiwi kushitakiwa ila huyu anatakiwa kufungwa jela. Pili, ni matendo ya viongozi wenyewe kwamba kiongozi ni kioo anachofanya ni rahisi kuigwa na wale anaowaongoza. Huwezi ukawa mwizi ukategemea wananchi hawataiba. Kwa hiyo itafika wakati kila aliye kwenye nafasi ya kuchota anajichotea kiasi chake. Ikishafika hapo hakuna nchi badala yeke, inakuwa imegawanywa maana watasema kama wao wanafanya sisi ni nani tusifanye hivi?

Niishauri serikali kwamba kama watu wamethibitika wamefuja na kuiba fedha za umma na mpaka sasa wako ofisini hawajawajibika Rais fukuza na washtakiwe kama wahujumu uchumi. Kuwahamisha ni kuhamisha matatizo maana wengine wanatumia uzoefu wao vibaya ni bora kuteua watu leo, kesho unafukuza kuliko kukaa na watu miaka yote lakini wanachokifanya ni kutumia uzoefu wao katika kufuja mali za umma, badala ya kujenga nchi wakati wanalipwa mishahara mizuri na mikubwa kuliko wengine ambao hawana nafasi ya kuiba.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR-ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mume kaungua mikono akipika sababu mke kachelewa kupika. Kosa la nani?



Na Adam Fungamwango

MLANGO wa ofisi yake uligongwa. Akaruhusu aliyegonga aingie. Alikuwa mwanamke aliyeonekana kuwa na shaka. Kwa jinsi alivyomwona hakuonekana kuwa ni mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda kile, akamkaribisha akae kwenye kiti.

Baada ya salamu akamuuliza ni nani, ametoka wapi na anahitaji msaada gani? Dada yule alijitambulisha kuwa yeye ni mmoja ya wake wa wafanyakazi wa idara yake na kuna shida imemleta pale.

Mkuu huyo wa idara si mwingine ila ni Juma Mrisho, maarufu kama 'Ngulimba wa Ngulimba.' Ni kiongozi wa bendi ya muziki wa dansi ya Urafiki Jazz iliyoanzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1970. Ilimilikiwa na Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, kikiwa na makao makuu yake maeneo ya Ubungo, Dar es Salaam, ambayo mpaka leo yanajulikana kama Urafiki. Jirani yake kuna Kituo cha Polisi ambacho nacho kinaitwa hivyo hivyo, Urafiki. Ngulimba wa Ngulimba, kiongozi na mwimbaji wa Urafiki Jazz alikuwa na ofisi yake kwa sababu alikuwa anahesabika kama mmoja wa wakuu wa idara wa kampuni hiyo. Idara yake ilikuwa ya muziki na utamaduni.

Dada aliyekuja kwa kiongozi huyo akaanza kutaja kilimchompeleka pale. Akaanza kueleza mambo ambayo anafanyiwa na mumewe. Akamwambia wamekuwa na ugomvi wa mara kwa mara na kisa ni mumewe kupenda kumwingilia kwenye majukumu yake kama mwanamke ikiwamo kupika.

Akasema anaporudi nyumbani na kukuta chakula bado hakijaiva, basi kwa hasira jukumu hilo anachukua yeye. Akamwambia Ngulimba wa Ngulimba kuwa kuna siku alifanya hivyo hivyo lakini kwa bahati mbaya akaungua mikono. Kwa hasira akamshushia mkong'oto wa nguvu na hilo likawa linajirudia mara kwa mara.

Mke anasema akapiga hesabu zake akaona kabla ya yote au kulifikisha mbali, akaona kwanza amwone kiongozi wa bendi anayopigia mumewe ili azungumze naye.

Kiongozi huyo baada ya kumsikiliza, akamwahidi kuwa atalifanyia kazi suala lake, wakaagana ikiwamo kumpa kidogo pesa ya nauli.

Kwa bahati nzuri wakati alipokuja pale mumewe hakuwapo kwa sababu ni mbali kidogo na wanapofanyia mazoezi. Bendi ilikuwa inafanyia mazoezi yake kwenye Ukumbi wa Jumba la Maendeleo Urafiki.

Ngulimba wa Ngulimba kama kiongozi wa bendi mwenye hekima, hakutaka kulisema hilo mazoezini, bali yalipomalizika alimwita mwanamuziki wake ofisini afike mara moja. Huko alimuuliza kama anamfahamu dada mmoja na akamtajia jina lake. Jamaa akajibu ni mkewe. Akaanza kumtajia kila shtala lake ambalo mkewe alikuja kumlalamikia.

Mwanamuziki huyo alishangaa, lakini naye ilibidi ajitetee. Akasema mkewe ana asili ya uvivu kwani mara kwa mara hujisahau na amekuwa akichelewa sana kupika na kila anaporudi anakuta chakula bado, lakini si kweli kwamba huwa anampiga na kuingia mwenyewe jikoni.

Kiongozi huyo anamtaka mwanamuziki wake aache tabia hiyo kama ni kweli anayo, na akamwambia abadilike na kumpa uhuru mkewe hata kama anachelewa kupika, akifika kama bado anaweza kufanya kazi zingine nyumbani, kulala au kutoka kidogo kwa ajili ya kusubiria chakula, lakini siyo kumnyang'anya mwiko na kuingia mwenyewe jikoni. Sakata hilo likasawazishwa hivyo.

Lakini mwanamuziki ni mwanamuziki tu. Kisa kile kilionekana kutotoka kwenye akili ya Ngulimba wa Ngulimba. Akaamua kukichukua kama kilivyo na kukitengenezea mashairi. Akamwita mwanamuziki wake aliyekuwa na mgogoro wa mkewe akampa asome mashairi yale. Jamaa akashangaa kwani anachokisoma ni kile kile ambacho kilishawahi kuwa mgogoro ambao ulisuluhishwa na kiongozi wake wa bendi.

Kiongozi akamwambia kisa chake ameamua kuutengenezea wimbo kwa sababu si yeye tu na mkewe ambao kitu kama hivi vinawatokea, bali ndani ya jamii vipo na vinatokana na sababu zile zile, hivyo ameamua kuliweka hadharani kwa ajili ya kuwaelemisha watu.

Akaomba idhini kwake na kumwambia hatotaja majina ya wahusika kwa sababu anachotaka ni ujumbe tu ufike kwa jamii, na yeye mwenyewe mhusika akaahidiwa kupewa kipande kikubwa cha kupiga chombo ndani ya wimbo huo. Jamaa akakubali.

Kisa hili cha kweli kabisa kilitokea katikati ya miaka ya 1970 na ndiyo chanzo cha wimbo uliotwao 'Kosa la Nani.'

Kupitia kisa kile kile cha mwanamuziki wake na mkewe, Ngulimba wa Ngulimba alipeleka mashairi yake mazoezini na yakaanza rasmi kukiwa hakuna yoyote aliyekuwa anajua chanzo cha wimbo huo unaofanyiwa mazoezi zaidi ya Ngulimba wa Ngulimba na mhusika mwenyewe.

Ulipokamilika ukaanza kupigwa kwenye kumbi mbalimbali na kuteka hisia za mashabiki wengi. Yote tisa, kumi iliporekodiwa ukawa ni mmoja wa wimbo bora wa bendi hiyo. Ukapendwa na kuombwa kwenye redio na kumbini, ukipeleka ujumbe na kuiasa jamii. Mtunzi alipita mle mle kwenye kisa cha mwanamuziki wake na mkewe, na mashairi yake yakaimbwa hivi.

"Wazee nimekuja kumshtaki mke mume wangu, amerudi kazini saa sita, njaa yamuuma, kaniuliza chakula nikamwambia bado, mara akaingia jikoni kaanza kupika.

Lakini bahati mbaya mikono ikaungua, mume kashika mkwaju kaanza kunitandika kosa la nani?

Mume wangu baba, anatabia mbaya sana kila nikianza kupika hunifuata jikoni ee

Mwongo sana mke wangu muongo haa, sina tabia kama hiyo wazee ha, hivyo ni visa vya mke wangu amezoea kudangaya, pia huchelewa kupika muongo haa."

Alichoongeza hapo mtunzi ni kwamba ameiweka kesi hii kama vile mke amekwenda kushtaki kwa wazee, na mume ameitwa hapo hapo akasomewa mashtaka yake na yeye akaanza kujitetea akimshushia shutuma mkewe pia. Hizi ndiyo kazi za wanamuziki wa dansi wa zamani.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




MEMSIKIA lakini wifi yenu?" Belo akawatumbulia macho dada zake nusu saa ya baada ya Husna kuondoka na watu kusambaratika.

"Mimi sikumuelewa ujue?" Tunda akajibu.

"Ndiyo hujamuelewa, lakini kwa jinsi alivyoonekana na alichoongea ni kama kuna kitu kakigundua au kakiona."

"Kitu gani hicho kaka? Si ulikuwa unamsikia hapa akisema kaka Dan ana mwanamke mwingine?"

"Siyo hivyo tu Tunda, kasema hata sisi tunajua kama Dan ana mwanamke mwingine. Na siyo kama kaja kuuliza, anachokuwa anakiongea ni kitu ambacho inaonekana ana uhakika nacho." Belo akawakazia macho dada zake.

"Kwa hiyo sisi ndiyo tunajua?" Akadakia Halima.

"Huwezi kujua, yule siyo mwendawazimu. Na mpaka kafikia hatua ile. Ukimsikiliza utagundua kuwa anakieleza kile ambacho anakielewa."

"Kwanza kanitisha mimi, nikajua kuna nini tena? Kaka kimemkuta nini huko Zenji, kumbe wivu."

"Tunda ee, tulia, mambo haya hayatuhusu, mambo ya mtu na mkewe watamalizana wenyewe, ukiingilia utaonekana mbea."

"Mbona na nyinyi kama mnanichanganya, mna kitu mnakijua?" Akauliza Belo.

"Mmmh, kaka na wewe, tujue nini, Dan alivyokuwa msiri yule, huku mwenyewe hatukumfahamu hadi alipotangaza ndoa."

"Nyinyi dada zangu mnadharau sana, angalia shemeji alivyokuja hapa, yaani kama mwendawazimu, nywele timtim, nguo haielewiki, hakuna mtu anayepagawa kiasi kile halafu awe amesikia tu, siyo kushuhudia, inabidi kwanza niwasiliane na Dan kujua kama kuna ukweli wa hili."

**************************************

"Nasema hivi sina shida na wewe. Nilikuwa nakusubiri urudi ili nikusanye kilicho changu niondoke usiseme nimetoroka sijui nimeenda wapi, hukunikuta, wala. Umerudi nakuachia nyumba naenda kwetu."

"Kwani kimetokea nini mke wangu?"

"Kelele bwana weee, mimi siyo mkeo! Mkeo ni yule aliyenipigia simu na kunitukana siku mbili mfululizo. Kanichamba, kuanzia kwenye unywele hadi ukucha. Hakuniacha kitu. Mwanamke anaongea utafikiri cherahani, hivi unavyoniona hapa niko mtupu. Sikuachwa kitu, nimenyonyolewa kama kuku kishingo. Yaani maneno niliyombiwa, hadi mimi mwenyewe najidharau."

**"Huwezi kujua, yule siyo mwendawazimu. Na mpaka kafikia hatua ile. Ukimsikiliza utagundua kuwa anakieleza kile ambacho anakielewa." "Kwanza kanitisha mimi, nikajua kuna nini tena? Kaka kimemkuta nini huko Zenji, kumbe wivu."**

Ndipo Dan alipoanza kuhisi kuna kitu ambacho si kawaida kilichotokea. Ni kwamba huenda mwanamke amekuja pale kugombana na mkewe. "Ni nani huyo?" Akajiuliza haraka haraka, lakini hakupata jibu.

"Hebu Husna nieleze kinachoelewka, ni nani alikuja hapa kukukorofisha?"

"Si afadhali angekuja hapa ungekuta tumepigana, tumepelekana polisi au tumeuana. Nimechambwa kwenye simu na hawara yako huyo uliyekuwa naye huko ulikokuwa."

Kichwa kilianza kumuuma Dan. "Mke wangu mimi nimetoka Zanzibar kikazi na wala huko sikuwa na mtu yeyote."

"Kamdanganye mtoto mdogo, asiyejua kitu. Labda unaona kama mimi nakudanganya. Ngoja nikwambie kila kitu halafu wewe ndiyo utaamua kusuka au kunyoa, lakini mimi nimeshaamua moja, kunyoa tu.

Yaani mimi ndiyo wa kuambiwa kuwa nimeolewa na wewe kwa sababu nimekulisha limbwata? Sina sura wala shepu ya kuolewa na wewe! Sipendezi blauzi, dela, kijora wala suruali, sipendezi sokoni wala 'super market'! Mimi sijui kupaka wanja wala 'lip stick', nimekung'ang'ania kama luba, mimi sijui kumlea mwanaume, sijui mahaba wala kunyenyekea, mimi mimi Husna..."

Baada ya kuongea maneno, akili yake ikarudi nyuma ikawa kama anayasikia tena maneno yale kwenye simu iliyopigwa siku ile.

Hakumruhusu mumewe amguse kumbembeleza. Akawa mkali kama pilipili.

Kitu pekee ambacho sasa alichokielewa ni kwamba kuna mfitini amefanya hivyo kwa makusudi kwa ajili ya kuivuruga ndoa yake. Ni nani? Bado akawa anajiuliza.

"Yaani ndoa yetu ina miezi miwili tu, tayari umeshawapa mahawara zako namba yangu ya simu kunitukana mimi? Tena uko nao huko, wananiambia tunaye hapa, wananiuliza tukupe uongee naye. Kwa hili mume wangu Dan umenikosea na sina msamaha, narudi kwetu, wala sio mbali, Mabibo kwenda Mburahati hata kwa miguu nakwenda. Sitaki senti tano yako, kwetu nitafika, sikuzaliwa juu ya miti mimi ninapo kwetu, na wala kwetu sijaua mtu." Yalimtoka maneno mtoto wa watu.

Kwa jinsi mke wake anavyoongea na hasira alizonazo, ilionekana hakuwa anaigiza, wala hayakuonekana ni maneno ya kuambiwa ni wazi kuwa kuna mwanamke wamempigia simu kweli na kumtolea maneno yasiyofaa.

Akawa anachanganua akili ni mwanamke gani aliyefanya hivyo kati ya wengi aliokuwa nao kabla ya kufungua ndoa na Husna.

"Na kwa taarifa yako simu yako uliyoninunulia nimeizima na kuifungia kabatini, siitaki tena unaweza kuitumia, na laini siitaki tena kwa sababu sitaki kuendelea kutukanwa, nimenunua simu mpya kwa hela yangu ya vikoba, na laini nimesajili nyingine kabisa. Hiyo kaa nayo, na laini nenda kawape hao wanaonitukana waendelee kunitukana vizuri."

Dan kila alipotaka kumbembeleza mkewe ili wayaongee na kuyamaliza ilikuwa ni kama anamwagia petroli kwenye moto wa gesi.

"Atakuwa ni Ziada." Akajisemea kimoyomoyo. Ndiyo, Ziada ndiye mmoja kati ya wapenzi wake ambaye alikuwa akipinga kwa nguvu zote asioe, badala yake ikiwezekana amuoe yeye.

"Ananitafutia nini huyu mwanamke? Si tumeshakubaliana mimi naoa na yeye akaniambia keshapata mchumba anataka aolewe?" Ni maswali aliyokuwa anajiuliza mwenyewe Dan kichwani.

Akili yake ilitua kwa mwanamke huyo kwa sababu yeye ndiye alikuwa akimpenda zaidi kwa dhati ya moyo wake, kuliko wanawake zake wengine ambao aliona kabisa walikuwa wanampendea pesa na si kingine. Na ndiye mwanamke pekee kati ya wapenzi wake ambao hakuja kwenye harusi yake kutokana na kuumizwa na hilo. Wengine walikubali yaishe na kuwa msitari wa mbele kwenye sherehe za harusi. Walicheza sana muziki, wakimwita Husna wifi. Sio kwamba walikuwa wanajuana, ila kila mmoja alikuja kivyake. Ni Dan peke ndiyo aliyekuwa anawafahamu wapenzi wake waliofika kwenye sherehe za harusi yake baada ya kukaa nao mmoja mmoja kikao kukubaliana kuwa sasa mapenzi yameisha na anafungua ukurasa mpya kwa kufunga ndoa. Ingawa kila mmoja alimuuliza kwa nini asingemuoa yeye, lakini mwishowe walisalimu amri na kuheshimu maamuzi yake. Kila mmoja aliahidi atafika kwenye harusi kwa moyo mweupe na kuanzia sasa waitane kaka na dada. Kwa Ziada ilikuwa ngumu sana. Alilia na kudai amedhulumiwa penzi.

"Ndiyo kaamua kunifanyia hivi? Atanitambua."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# DUDE AMLILIA MAKABILA KUMFANYIA MBAYA

MSANII wa filamu, Dude, amesema alichofanyiwa na mwanamuziki Dulla makabila, ni jambo lisolosameheka kwani limemuumiza yeye binafsi, rafiki na familia yake.

Dulla Makabila jana aliposti katika akaunti yake ya Instagram kwamba Dude amefariki Dunia, kama sehemu ya kuadhimisha siku ya wajinga duniani.

"Nimechanganyiwa sana, simu yangu ilielemewa na watu ambao walitaka kujua ukweli kama nimekufa au niko hai, huyu Dulla Makabila mimi sina utani naye nashangaa kwa nini kasema kitu kama hiki ambacho kimewaumiza watu," amesema Dude.

Amesema anashindwa kumtafuta msanii huyo kwa ajili ya kumwambia jambo lolote, kutokana na akili yake kuchanganyikiwa kwa taarifa hizo ambazo sio sahihi.



# *Rayvanny aibua minong'ono*

MSANII wa Bongo Fleva, Rayvanny ameachia video ya kibao kipya 'Forever' ambayo ndani yake amemshirikisha mama mtoto wake.

Kumshirikisha Fahma katika video hiyo kumeibua minong'ono kwamba wawili hao wameamua kurudiana baada ya penzi lao kuvunjika muda mrefu.

Rayvanny ameonekana akiwa katika hisia kali katika wimbo huo, huku akimruhusu mama wa mtoto wake kufanya yote anayopenda.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAMTAKA OSIMHEN

CHELSEA imeingia katika mbio za kuwania huduma ya mshambuliaji wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24 baada ya msimu huu kumalizika. (***Evening Standard***)

### BALDE ATAJWA CHELSEA

CHELSEA wanajipanga kuwasilisha ombi la kumnunua beki wa kushoto wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Alejandro Balde, mwenye umri wa miaka 19, kuwa msaidizi wa beki wao wa England, Ben Chilwell (26). (***Sport***)

### KAI KUREJEA BAYERN

BAYERN Munich wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Kai Havertz, mwenye umri wa miaka 23, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani akionyesha anahitaji kungana tena na kocha wake wa zamani, Thomas Tuchel. (***90Min***)

### PSG KUMBAKIZA MESSI

KLABU ya Paris St-Germain imemwambia, Lionel Messi, watalipa kiasi chochote cha fedha kinachohitajika ili kumbakisha mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 35, huku kukiwa na ripoti Barcelona wamewasiliana na Messi kuhusu uwezekano wa kurejea. (Mundo Deportivo)

### ARSENAL YAMTAKA TCHOUAMENI

ARSENAL inamtaka kiungo wa kati wa Real Madrid, Aurelien Tchouameni, ili kuboresha kikosi chao msimu wa joto, huku Liverpool pia ikidaiwa kumtaka Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 23. (***El Nacional***)

### LIVERPOOL KUMWAGA MPUNGA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema klabu hiyo imekuwa na shughuli nyingi wakati wa mapumziko ya kimataifa ikipanga malengo ya msimu wa joto na iko tayari kutumia fedha nyingi katika soko la usajili. (***Mirror***)

### AUBAMEYANG AITAKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye umri wa miaka 33 anataka kurejea Barcelona, lakini The Blues hao hawataki kumuuza mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Gabon. (***Sport***)

### DE GEA ANUKIA ROMA

AS Roma wanafikiria kumnunua mlinda mlango wa Manchester United, David de Gea wakati Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 32 mkataba wake ukikamilika msimu wa joto. (***Fichajes***)

### AYEW KIMEELEWEKA PALACE

WACHEZAJI wawili wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya Ghana, Jeffrey Schlupp mwenye umri wa miaka 30, na Jordan Ayew (31), wameweka saini katika mikataba mipya. (***Athletic***)

### KEITA AKARIBIA MILAN

AC Milan wamepewa ofa ya kiungo wa kati wa Guinea, Naby Keita, mwenye umri wa miaka 28 kabla ya kuondoka Liverpool msimu huu wakati mkataba wake utakapomalizika. (***Calciomo***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA, BABA MESSI WAKUTANA

**Bosi wa klabu hiyo akiri wanapenda kuona nyota huyo anarejea...**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imekiri imewasiliana na Lionel Messi kuhusu kumrejesha klabuni hapo mkataba wake na Paris Saint-Germain utakapokamilika Juni, mwaka huu.

Makamu wa Rais wa Barca, Rafa Yuste, alithibitisha Ijumaa klabu hiyo inaangalia uwezekano wa kumsajili tena Messi, ambaye aliondoka kwenda PSG mwaka 2021, huku Kocha, Xavi Hernandez, baadaye akiongeza anatumaini kumwona nahodha huyo wa Argentina akirejea tena hapo Camp Nou.

"Bado nina huzuni hangeweza kuendelea hapa," Yuste alisema katika mkutano na wanahabari.

"Bila shaka ningependa arudi, kwa sababu ya kile anachowakilisha katika kiwango cha michezo, kijamii na kiuchumi.

**"Tunawasiliana na kambi ya Messi, ndiyo. Hadithi nzuri zinapaswa kuwa na mwisho mwema, na kuna upendo wa pande zote mbili."**

Messi mwenye umri wa miaka 35, aliondoka miaka miwili iliyopita baada ya miongo miwili ya kukaa Katalunya kwa sababu Barca hawakuweza kumudu kuongeza mkataba wake.

Upande wa kifedha wa kurudi yoyote msimu huu wa joto unabaki kuwa kikwazo.

Barca wanahitaji kuondoa zaidi ya euro milioni 150 kwenye matumizi yao ya kila mwaka, au kutafuta fedha kupitia uhamisho, ili kuzingatia kanuni za kiuchumi za LaLiga na kusajili wachezaji wapya.

"Bado tuna miezi miwili ya kufanya kazi kwa bidii kuwasilisha mpango wetu wa mapato na uendelevu kwa Rais wa LaLiga, Javier Tebas," aliongeza Yuste alipoulizwa kama kumrejesha Messi inawezekana kweli.

"Sipendi kuzungumza juu ya Leo kwa sababu ni mchezaji wa PSG, lakini ikiwa masharti yote yatatimizwa, tuko wazi kwa uwezekano huo. Rais wa Barca, Joan Laporta, amekuwa na baba yake Leo, na kuna uhusiano mzuri."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 536,

MECHI KALI
NEWCASTLE
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.34
X | 3.20
2 | 2.85

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POGBA MAMBO MAGUMU JUVENTUS




**TURIN,** Italia

KOCHA Massimiliano Allegri hana uhakika ni lini Paul Pogba atarejea uwanjani baada ya majeraha yake ya hivi majuzi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amekuwa na wakati mgumu wa mambo tangu arejee Juventus kutoka Manchester United Julai, mwaka jana, akicheza kwa dakika 34 tu katika mechi mbili alizotokea benchi.

Pogba alionekana kusahau matatizo yake ya majeraha wakati akicheza mechi za mfululizo dhidi ya Torino na Roma hapo Februari 28 na Machi 5, mwaka huu, mara zote mbili kama mchezaji wa akiba.

Lakini alitolewa katika mechi iliyofuata ya Ligi ya Europa wakati Juventus ilipocheza dhidi ya Freiburg, kutokana na kuchelewa kufika kwenye kikao cha timu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 hajaonekana tangu wakati huo baada ya kupata tatizo jipya la misuli alipokuwa akipiga mpira wa adhabu kwenye mazoezi.

"Kwa sasa sijui ni lini atapatikana tena," alisema Allegri akiwaambia waandishi wa habari jana.

"Anafanya mazoezi, lakini kwa sasa ni vigumu kusema.

"Mchezaji huyo yuko sawa, lakini tunasubiri kuona jinsi goti lake litakavyokuwa baada ya kushiriki katika mazoezi."

# Spurs haipo katika mgogoro




**LONDON,** England

CRISTIAN Stellini amesisitiza Tottenham "haiko kwenye mgogoro" licha ya Antonio Conte kuondoka katika klabu hiyo.

Conte aliondoka Spurs kwa makubaliano Jumapili iliyopita, wiki moja baada ya kutokea sare ya mabao 3-3 na Southampton ambayo inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea aliwataja wachezaji wake "wabinafsi" na kutilia shaka klabu hiyo kukosa fedha wakati Daniel Levy alipokuwa mwenyekiti katika ghasia ambazo hatimaye zilimgharimu kibarua chake, huku msaidizi wake, Stellini akichukua mikoba hadi mwisho wa msimu.

Conte anakuwa kocha wa tatu wa Spurs kuondolewa majukumu yake tangu Mauricio Pochettino, ambaye aliiongoza Spurs kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Mkurugenzi Mtendaji, Fabio Paratici pia ameachana na jukumu lake wakati klabu hiyo ikisubiri matokeo ya rufaa yake dhidi ya kufungiwa kujihusisha na soka duniani kote kufuatia uamuzi wa FIFA wa kuongeza marufuku yake ya awali ya miezi 30 kutokana na ufujaji wa wa fedha akiwa Juventus.

Hata hivyo Stellini, ambaye sasa ana jukumu la kusimamia michezo 10 ya mwisho ya msimu huu huku Spurs ikipania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, hakubaliani kuwa klabu hiyo iko kwenye msukosuko, licha ya mashabiki wa Tottenham kuelezea kuwa timu yao haipo sawa.

,262,050

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/04/23 | 21:15 | Perugia vs Reggina | 2.52 | 2.94 | 2.83 |
| 02. 05/04/23 | 21:45 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 2.29 | 3.60 | 2.90 |
| 03. 05/04/23 | 22:00 | Barcelona vs Real Madrid | 2.29 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 05/04/23 | 22:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.25 | 2.22 |
| 05. 06/04/23 | 01:00 | Danubio FC vs SC Emelec | 2.38 | 3.05 | 2.84 |
| 06. 06/04/23 | 02:00 | Huachipato vs Union Espanola | 2.40 | 3.21 | 2.69 |
| 07. 06/04/23 | 03:05 | Pumas De Tabasco vs Zacatepec | 2.89 | 3.36 | 2.19 |
| 08. 06/04/23 | 05:00 | Deportivo Pereira vs Colo Colo | 2.58 | 3.08 | 2.58 |
| 09. 06/04/23 | 19:00 | Slask Wroclaw vs GKS Piast Gliwice | 2.43 | 3.09 | 2.67 |
| 10. 06/04/23 | 22:15 | El Ittihad Alexandria vs Coca Cola | 2.86 | 2.91 | 2.56 |
| 11.07/04/23 | 03:00 | FBC Melgar vs Olimpia Asuncion | 2.25 | 3.13 | 2.98 |
| 12. 07/04/23 | 03:00 | CA Tigre vs Sao Paulo | 2.54 | 3.06 | 2.64 |
| 13. 07/04/23 | 08:00 | Western United vs Central Coast Mariners | 2.68 | 3.26 | 2.47 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 02/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 1368 | GO Ahead Eagles vs Ajax | 7.42 | 5.01 | 1.32 |
| 13:30 | 4503 | Bologna vs Udinese | 2.20 | 3.20 | 3.10 |
| 14:00 | 5425 | Lille vs Lorient | 1.36 | 4.80 | 6.80 |
| 15:00 | 1889 | Celta Vigo vs Almeria | 1.53 | 3.89 | 5.59 |
| 15:00 | 3748 | Rubin Kazan vs Veles | 1.30 | 4.51 | 8.40 |
| 15:30 | 1968 | Sparta Rotterdam vs Feyenoord | 5.39 | 3.75 | 1.57 |
| 15:30 | 5712 | Utrecht vs FC Volendam | 1.39 | 4.80 | 6.19 |
| 16:00 | 1125 | Brest vs Toulouse | 2.71 | 3.26 | 2.42 |
| 16:00 | 2900 | Norrkoping vs Sirius FK | 1.82 | 3.54 | 3.60 |
| 16:00 | 3130 | Nantes vs Reims | 2.95 | 3.19 | 2.29 |
| 16:00 | 4045 | West Ham vs Southampton | 1.72 | 3.45 | 4.59 |
| 16:00 | 4249 | Clermont Foot vs AC Ajaccio | 2.09 | 3.06 | 3.51 |
| 16:00 | 4995 | Spezia vs Salernitana | 2.28 | 3.15 | 3.00 |
| 16:00 | 5214 | Angers vs Nice | 5.60 | 3.70 | 1.56 |
| 16:00 | 5442 | Monza vs Lazio | 3.50 | 3.15 | 2.06 |
| 16:00 | 5736 | HNK Rijeka vs NK Osijek | 2.11 | 3.12 | 3.17 |
| 16:30 | 3452 | Fakel vs CSKA Moscow | 4.61 | 3.67 | 1.67 |
| 16:30 | 4751 | FC Koln vs Monchengladbach | 2.18 | 3.41 | 2.95 |
| 17:00 | 2229 | Brondby vs Viborg FF | 1.90 | 3.50 | 3.81 |
| 17:00 | 2311 | Eupen vs Anderlecht | 3.82 | 3.67 | 1.82 |
| 17:15 | 3827 | Real Madrid vs Valladolid | 1.23 | 5.77 | 9.92 |
| 17:30 | 2497 | GD Chaves vs Sporting Braga | 4.53 | 3.72 | 1.68 |
| 17:30 | 5263 | Maritimo vs Boavista | 2.44 | 3.07 | 2.87 |
| 17:45 | 4546 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.11 | 3.30 | 3.20 |
| 18:00 | 2224 | Slavia Mozyr vs Dinamo Minsk | 4.89 | 3.64 | 1.61 |
| 18:00 | 5047 | Saint George FC vs Ethiopia Electricity | 1.29 | 4.30 | 7.60 |
| 18:05 | 5088 | Monaco vs Strasbourg | 1.50 | 4.20 | 5.40 |
| 18:30 | 1323 | TS Galaxy FC vs Maritzburg Utd | 2.07 | 3.08 | 3.55 |
| 18:30 | 1700 | IFK Goteborg vs IFK Varnamo | 1.82 | 3.44 | 3.70 |
| 18:30 | 2645 | Newcastle vs Manchester Utd | 2.34 | 3.20 | 2.85 |
| 18:30 | 4198 | Werder Bremen vs Hoffenheim | 2.26 | 3.39 | 2.84 |
| 18:30 | 4396 | Halmstads BK vs AIK Football | 3.28 | 3.13 | 2.06 |
| 19:00 | 1392 | Lokomotiva Zagreb vs Vsnk Varazdin | 1.87 | 3.35 | 3.60 |
| 19:00 | 2099 | Roma vs Sampdoria | 1.41 | 4.11 | 7.21 |
| 19:00 | 2962 | Radnicki Nis vs Cukaricki St | 3.03 | 2.98 | 2.25 |
| 19:00 | 4711 | Levadia Tallinn vs Kuressaare | 1.35 | 4.66 | 7.04 |
| 19:00 | 5566 | Rostov vs Torpedo Moscow | 1.55 | 3.84 | 5.47 |
| 19:30 | 1132 | Villarreal vs Real Sociedad | 2.32 | 3.04 | 3.04 |
| 19:30 | 5026 | Mechelen vs Brugge | 3.52 | 3.62 | 1.91 |
| 20:00 | 2697 | Bohemians vs Slovacko | 2.56 | 3.44 | 2.51 |
| 20:00 | 2805 | Rio Ave vs Benfica | 7.82 | 4.82 | 1.33 |
| 20:30 | 4828 | Fenerbahce vs Besiktas | 1.87 | 3.63 | 3.63 |
| 21:00 | 2264 | Ahli Al-Fujirah vs AL Jazira AL Hamra | 1.97 | 3.65 | 3.03 |
| 21:00 | 4893 | Hatta Club vs Masafi | 1.49 | 4.22 | 4.94 |
| 21:00 | 5992 | Al Nasr Dubai vs Ittihad Kalba | 2.04 | 3.39 | 3.08 |
| 21:45 | 3418 | Napoli vs AC Milan | 1.88 | 3.28 | 3.96 |
| 21:45 | 4288 | Paris St Germain vs Lyon | 1.46 | 4.41 | 5.63 |
| 21:45 | 5061 | Bahrain Club vs Manama Club | 4.46 | 3.52 | 1.69 |
| 22:00 | 2297 | Atletico Madrid vs Betis | 1.51 | 3.94 | 5.79 |
| 22:30 | 5756 | Porto vs Portimonense | 1.15 | 6.84 | 15.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KAGERA SUGAR YATAMBA KUZIKA NDOTO ZA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

BENCHI la ufundi la Kagera Sugar limesema linawasubiri kwa hamu Yanga kwa ajili ya kukutana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Aprili 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga itawakaribisha Kagera Sugar ikiwa bado na joto la mechi ya kimataifa za Kombe la Shirikisho Afrika.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mecky Maxime, amesema hawana wasiwasi kwa sababu watakutana na Yanga ikiwa imerejea na uchovu wa safari ya kutoka Lubumbashi wakati wao wamepata muda mrefu wa kufanya maandalizi.

"Kikubwa sisi tunajiandaa kwa ajili ya kuchukua pointi tatu kwao, tunajua tunacheza na timu ya aina gani, inayoongoza ligi na inataka kutetea ubingwa wake, hivyo tunajua tunakwenda kukutana na ugumu kiasi gani, ndiyo maana tumekuwa tunajiandaa kikamilifu ili tumalizane nao," alisema Maxime.

Beki huyo wa zamani wa Taifa Stars na Mtibwa Sugar alisema kikosi chake kimerejea kambini na anaamini muda wa mapumziko waliopata umesaidia kurejenga nguvu za wachezaji wake.

"Kikosi chetu kimerejea kambini baada ya mapumziko ya muda mfupi kupisha michezo ya kimataifa, ila tumeendelea kuimarika, tunahitaji kumaliza mechi zilizosalia kwa kupata matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

Kagera Sugar ipo katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 32 baada ya kucheza mechi 25 za msimu huu.



Wachezaji vijana wa mpira wa miguu wakifanya mazoezi ili kukuza vipaji vyao kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete Youth Park, Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Simba SC yajivunia kiwango Morocco

INATOKA UK 24

makosa ya mchezaji mmoja mmoja.

Mara ya mwisho Raja Casablanca kufungwa goli kwenye uwanja wao katika mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika ilikuwa Aprili 22, mwaka jana walipocheza dhidi ya Al Ahly katika hatua ya robo fainali, hivyo kitendo cha Simba kupata goli ni ishara kuwa eneo letu la ushambuliaji limeimarika. Sasa tunasonga mbele zimebaki siku 20 tucheze robo fainali maandalizi yanaanza sasa," alisema meneja huyo.

Kipigo hicho kinaifanya Simba kwa mara ya kwanza kupoteza mechi mbili dhidi ya timu moja kwa misimu mitano ambayo ilicheza mechi za kimataifa.

Februari 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ilifungwa mabao 3-0 na Raja Casablanca, Hamza Khabba, ambaye alifunga bao la kwanza kwenye mechi hiyo ndiye aliyepachika mabao mawili katika mchezo wa usiku wa kuamkia jana na lingine likipachikwa na Mohamed Boulacsout wakati Baleke akifunga bao pekee kwa upande wa Simba.

Raja Casablaca yenye pointi 16 imemaliza hatua hiyo ikiwa kinara wa Kundi C ikifuatiwa na Simba yenye pointi tisa, Horoya ya Guinea wana pointi saba na Vipers FC ya Uganda ikiburuza mkia na pointi mbili mkononi.

# Michezo

UK. 21

Nipashe

Jumapili Aprili 2, 2023






Barcelona, baba Messi wakutana




Kocha wa viungo wa Yanga, Helmy Gueldich (katikati), akiongoza mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji TP Mazembe itakayochezwa leo kwenye uwanja unaomilikiwa na klabu hiyo ulioko katika mji wa Lubumbashi, **DRC. PICHA: YANGA SC**

# Yanga, Mazembe hesabu uwanjani

**Na Saada Akida**

## ●●● Nabi asisitiza anataka kuongoza kundi lao na kuweka rekodi ya...

SISI ni wakubwa Tanzania, hayo ni maneno ya mabingwa na vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga kuelekea mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe itakayochezwa leo mjini Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mechi hiyo ya kukamilisha ratiba kwa sababu timu zote mbili zimeshakata tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo itachezwa kuanzia 10:00 jioni kwa saa za Tanzania.

Yanga itashuka dimbani ikisaka ushindi wa kwanza ugenini katika hatua hiyo baada ya kupoteza mabao 2-0 dhidi ya US Monastir huko Tunisia na kuambulia sare ya goli 1-1 ilipowafuata AS de Real Bamako nchini Mali.

Takwimu zinaonyesha vigogo hao wamekuwa na nyakati ngumu ugenini, wakifunga bao moja na kuambulia pointi moja ndani ya dakika 180.

Mshambuliaji nyota wa Yanga, Fiston Mayele alifunga bao katika mechi dhidi ya Real Bamako lakini wawakilishi hao wakiwa na matokeo bora kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa msimu huu.

Endapo Yanga itapata ushindi leo, itakuwa na nafasi nzuri ya kuongoza Kundi D ikifuatiwa na US Monastir ambayo pia imetinga hatua ya robo fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema wamepata siku mbili nzuri za kufanya mazoezi kwenye Uwanja unaomilikiwa na klabu hiyo ya TP Mazembe.

Nabi alisema walikuwa na safari ndefu ya maandalizi na wamejiandaa vizuri kuingia katika mchezo huo wa mwisho wa hatua ya makundi wakiwa na lengo moja la kusaka ushindi.

"Tumefurahi kufanikisha malengo ya timu ya kufuzu kucheza hatua ya robo fainali, bado kuna malengo yanapaswa kuendelea kutimia ikiwa ni pamoja na kupata ushindi katika mchezo wetu wa kesho (leo)," alisema na aliongeza;

Kitu ambacho tumekifanya kwa sasa ni jitihada kwenye maandalizi ya kuwakabili wapinzani kwa nidhamu kubwa jambo litakalosaidia kutupa matokeo bora ugenini," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza Mayele na Stephen Aziz Ki hawakuwa sehemu ya wachezaji waliofanya maandalizi ya pamoja na wenzao tangu walipofika Lubumbashi kutokana na kuwa kwenye majukumu ya kimataifa, lakini anaamini wako tayari kwa mapambano.

Alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kutokana na rekodi nzuri ya wapinzani wao wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani ambao walipata ushindi walipowakaribisha Real Bamako.

"Tunahitaji kupata pointi tatu muhimu katika mchezo wetu wa mwisho, licha ya kufuzu bado tunatakiwa kucheza kwa nidhamu kubwa kwa sababu tunataka kuongoza katika kundi letu," alisema kocha huyo.

Naye beki wa timu hiyo, Dickson Job, alisema wamejipanga vizuri na wamepewa maelekezo mazuri na benchi la ufundi kwa ajili ya kuhakikisha wanaendeleza kasi ya ushindi waliyokuwa nayo.

"Kazi iliyosalia ni sisi kukamilisha dakika 90 za kusaka alama tatu, tunatambua hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu wenzetu wako nyumbani kwao, kila mtu anahitaji kutumia vizuri uwanja wa nyumbani kama ilivyo kwetu, kikubwa niseme tuko tayari kuwavaa TP Mazembe," alisema Job.

Ikirejea nchini, Yanga itaanza maandalizi ya kuwakaribisha Geita Gold FC katika mechi ya Kombe la FA itakayochezwa Aprili 8, mwaka huu.

# Simba SC yajivunia kiwango Morocco

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kufungwa mabao 3-1 dhidi ya wenyeji, Raja Casablanca katika mechi ya mwisho ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba imesema inajivunia kiwango kikubwa kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo huo.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' aliliambia gazeti hili licha ya makosa madogo madogo yaliyojitokeza ya mchezaji mmoja mmoja, bado kikosi chake kilionyesha ukomavu katika mechi hiyo iliyokuwa ya kukamilisha ratiba.

Robertinho pia aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuonyesha ubora kila walipokuwa na mpira na wakati wakikosa waliamka na kuwabana wapinzani wao.

Kocha huyo alisema alilazimika kubadilisha mfumo wa uchezaji katika kikosi chake kutokana na aina ya mpinzani na ugumu wa mechi husika.

"Nilimchezesha Jean Baleke kama straika pekee kule mbele, na kazi yake ilikuwa ni kuzishambulia nafasi au kusaka nafasi zilizo wazi wakati akiwa hana mpira, na zilifanya kazi, bao lilipatikana lingine lilikataliwa. Kusema kweli ninavyoona, siku za usoni Simba itakuwa na kikosi bora kabisa," alisema Robertinho.

Aliongeza anaamini changamoto walizokutana nao katika mechi hiyo, zitawasaidia kuelekea mchezo wa robo fainali.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema bila kujali matokeo lakini wachezaji wa timu hiyo wamecheza kwa nidhamu kubwa na tayari wamepata picha ya kucheza mechi ya robo fainali watakapokuwa ugenini.

"Bila kujali matokeo, tumecheza kikubwa sana, nidhamu yetu ya mchezo ilikua juu mno kwenye kukaba na kushambulia, tumepata picha tunaenda kucheza vipi robo fainali yetu, na benchi la ufundi limeona ni wapi watafanyia kazi hasa kwenye kuepuka


INAENDELEA UK 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >